Nipashe
Ijumaa Agosti 11, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581399
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII




UKURASA 11

SUPA JACKPOT
TZS. 1,142,132,257
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



MAZUNGUMZO MAALUM

## **Dorothy** wa ACT asema atawania urais mwaka 2025

UKURASA 4

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Korti Kuu yabariki mkataba Bandari

• **Kina** Mwabukusi wajipanga kukata rufani...*Endelea ukurasa wa 3*





Wananchi wakiwa wamekusanyika nje ya Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya jana, wakisubiri uamuzi wa kesi ya kupinga mkataba wa uwekezaji wa Bandari. **Picha ndogo:** Mwanasheria Alphonce Lusako, ambaye ni mlalamikaji katika shauri hilo, akizungumzia kuhusu kutoridhishwa na uamuzi wa mahakama wa kulitupilia mbali shauri hilo. **PICHA: KULWA MZEE**

## Samia ataka Watanzania watambuliwe kwa namba



UKURASA 2

## Mitambo ya kupandikiza mimba yatua bandarini



UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA, YANGA RASMI KUKUTANA JUMAPILI** UK.24

**KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA




Rais Samia Suluhu Hassan akiwa amevaa kifaa maalum cha kumwezesha kuona kwa ukaribu matukio mbalimbali Duniani kijulikanacho kama Teknolojia Ukweli Halisi, baada ya kuzindua mtandao wenye kasi ya 5G katika Kituo cha Mkongo wa Mawasiliano Baharini cha Airtel Tanzania, Mbezi Tangi Bovu, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye na Mtendaji Mkuu wa Airtel Tanzania, Dinesh Balsingh. **PICHA: IKULU**

# Mitambo upandikizaji mimba yatua nchini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MITAMBO ya huduma za upandikizaji mimba katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) imewasili nchini na imegharimu Sh. bilioni moja.

Wakati mitambo hiyo ikiwasili nchini, watu 128 hadi sasa wamepandikiziwa maputo tumboni ili kupunguza uzito huku watatu wakishindwa kukaa nayo.

Akizungumza jana jijini hapa kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali na mwelekeo wa mwaka wa fedha 2023/24, Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Mohamed Janabi, alisema hospitali hiyo imenunua mitambo hiyo na sasa wanaendelea na mchakato wa kuitoa bandarini.

"Sisi ni sehemu ya serikali. Mitambo imenunuliwa kwa gharama ya Sh. bilioni moja hadi ifungwe na kukabidhiwa. Tuvute subira na nina uhakika kabla ya kufika mwisho wa mwaka huu, kila kitakuwa tayari kwa sababu jengo lipo tayari litakuwa la peke yake kabisa na la kisasa lipo karibu na kanisa," alisema.

Alisema watalaamu wamesomeshwa watakao toa huduma hiyo ambao wanasubiri mitambo na kwa mwanzoni watashirikiana na wenye utalaamu na uzoefu mkubwa kwenye hilo.

Alibainisha kuwa gharama za upandikizaji hazitakuwa kama za nje ya nchi na kuwahimiza Watanzania kukata bima kwa kuwa huduma za kibobezi ni gharama kubwa.

Kuhusu puto, alisema huduma hiyo imefanywa siku za wikiendi na wanapandikizwa siku hiyo hiyo.

"Hawa watatu kwenye hii miili yetu nikiingiza kitu chochote mwili utasema kuna kitu kigeni kimeingia mwili unashtuka. Ukiingizwa puto siku ya kwanza, dalili zake ni kama mwanamke anavyoshika ujauzito. Anajisikia kichefuchefu na baada ya muda hutulia lakini hawa walishindwa kuvumilia.

"Puto tunaingiza kupitia mdomoni kwa kutazama kwenye kamera hadi linafika tumboni na kuna dawa ya kimiminika tunaweka mililita 500. Unachofanya unapunguza ukubwa wa tumbo. Ukila kidogo unajisikia umeshiba, unakaa nalo miezi minane," alisema.

Prof.Janabi alisema wameanza kuwatoa wengine ambao wamefikisha muda huo na wanaendelea vizuri.

"Mgonjwa ambaye ana kilo ndogo tuliyempokea ni mwenye kilo 110 na wenye kilo nyingi ni 200," alisema.

Alihimiza Watanzania kula kwa mpango ili kujiepusha na ulaji kupita kiasi unaosababisha magonjwa yasiyo ya kuambukiza yakiwamo kisukari na chakula hatari zaidi ni sukari na wanga.

Kadhalika, alisema katika mwaka 2023/24, alisema hospitali hiyo itajengwa upya kwa kubomolewa baadhi ya majengo ambapo zaidi ya Sh.Bilioni 600 zimetengwa.

Awali, alisema katika kupunguza msongamano wa watu kwenye hospitali hiyo ilifanya tathimini na kubaini kuwa kwa siku moja eneo hilo wanaingia watu 20,000 na magari 3,500.

"Tathmini hiyo ilionyesha kuwa kuna baadhi ya watu wanaegesha magari yao ndani kutokana na usalama uliopo, kutokuwepo mfumo wa malipo ya maegesho ambapo wakishaegesha huenda kufanya shughuli zao Kariakoo au mjini," alisema.

Prof. Janabi alisema hali hiyo iliwalazimu kuanzisha utaratibu wa kulipia huduma ya maegesho ili isaidie kupunguza msongamano wa magari ndani ya hospitali na wanatozwa Sh.500.

Pia alisema wamepunguza idadi ya ndugu wanaofika kusalimia wagonjwa waliolazwa kutoka watano kwa wakati mmoja hadi wawili asubuhi, mmoja mchana na wawili jioni.

**LINDI FORESTS LIMITED**
**The companies Act, 2002 (Section 334)**
**MEMBER'S VOLUNTARY WINDING – UP**

**NOTICE IS HEREBY GIVEN** to the general public that **TANGA FORESTS LIMITED** a company with registration number **54989** dully convened a meeting on 15th July, 2023 and passed a special resolution in accordance to section 333 (1) (b) of the Companies Act, 2002 that the company be wound up voluntarily.

All parties concerned and who have claims are hereby notified to submit their claims in a closed envelop within 30 days to **GODFREY BASIL MRAMBA of Basil & Alred, Ace Building, Haile Selassie Road, P.O. Box 78661, Dar es salaam, Tanzania,** who is appointed Liquidator of the Company.

**Any claims lodged after 30 days from this publication will not be considered for admission.**

**GODFREY BASIL MRAMBA**
**Liquidator**
**For TANGA FORESTS LIMITED**

# Samia ataka Watanzania watambuliwe kwa namba

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan ameziagiza taasisi zinazotoa huduma za kibenki, Wizara za Elimu na Afya, kushirikiana na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), kuanzisha utaratibu wa kutoa huduma kwa watanzania kwa kutumia namba moja.

Alisema utaratibu huo utarahisisha utekelezaji wa majukumu yao na kuboresha usalama nchini kwa kuwa kila Mtanzania atakuwa na namba ambayo ikiingizwa kwenye mfumo katika taasisi hizo taarifa zake zinasomeka.

Alitoa agizo hilo jana, jijini Dar es Salaam katika hafla ya uzinduzi wa kituo cha mkongo wa mawasiliano baharini wa '2 Afrika' na teknolojia ya mawasiliano ya kasi ya 5G vya Kampuni ya Simu ya Airtel.

Agizo hilo limekuja ikiwa ni miezi miwili tangu Ripoti ya Tume ya kuangalia namna ya kuboresha Taasisi za Haki Jinai nchini kupendekeza huduma za kijamii na kibiashara zifungamanishwe na mifumo ya utambuzi na usajili ikiwamo Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) na NIDA ili kila mwananchi awe na namba moja ya utambuzi.

"Atakapoandikwa Samia Suluhu ni namba 20 ndani ya Tanzania basi taarifa zangu zote, taasisi zote zikivuta hiyo lije jina la Samia Suluhu yule yule, taarifa zile zile," aliagiza.

Alimwagiza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa azisimamie Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Mamlaka ya Serikali Mtandao (E-Government) kuboresha huduma ya intaneti katika taaisi za serikali ziachane na utoaji wa huduma kizamani unaochelewesha utekelezaji wa majukumu yao.

Pia, aliwataka watanzania kuhakikisha taarifa walizozitoa NIDA zina tofauti waende kurekebisha ili watambulike kupitia taarifa hizo.

Rais Samia aliagiza Wizara ya Habari kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuharakisha mchakato wa matokeo ya utafiti utakaotoa bei za mwelekeo wa ujumbe, takwimu na simu kwa mwaka 2023 hadi 2027 ili kuona mwelekeo wa mtandao wa 5G.

Mkongo huo ni muhimu katika maendeleo ya mawasiliano na teknolojia na utaleta mapinduzi makubwa katika sekta ya mawasiliano nchini.

Serikali kwa kutambua umuhimu wa TEHAMA hasa wakati huu ambao teknolojia inakuwa kwa kasi imejizatiti kuweka mazingira wezeshi kwa kutoa huduma za uwekezaji na kujenga miundombinu ya mawasiliano.

"Hivi karibuni tumeanza mradi wa ujenzi wa minara mipya 758 kwa ajili ya kupanua wigo wa mawasiliano ambao utawanufaisha zaidi ya watanzania milioni nane kote nchini, mijini na vijijini," alisema Rais.

Alisema katika mradi huo serikali imepunguza gharama ya kuweka mkongo kwenye hifadhi za barabara kutoka Dola za Kimarekani 1,000 hadi 100 tofauti ya dola 900 ili usambazwe kwa haraka.

Pia, imepunguza gharama za awali za upitishaji wa mkongo huo kutoka Dola 1,000 hadi 2000, ili kupanua huduma za intaneti na kuwafikia asilimia 85 ya watanzania kwa bei nafuu ifikapo mwaka 2025.

Tawimu zilizotolewa Machi mwaka huu na Mamlaka ya Mawasiliano nchini (TCRA), zinaonyesha kuna laini za milioni 61 zilizosajiliwa, kati ya hizo milioni 33 peke zinazotumia huduma ya intaneti kutokana na changamoto ya upatikanaji wa vifaa janja ambavyo vina gharama kubwa.

Huduma hiyo pia itasaidia kufanya matangazo ya utalii kwa kutumia mtandao huo wa 5G na kuvutia wengi kuja kutembelea nchini, kuboresha huduma za afya na kuleta maendeleo katika sekta elimu.

Aidha, alisema kuongezeka kwa mkongo huo kutaleta ushindani nchini na kukuza ubora wa intaneti na kushuka kwa gharama za mawasiliano kwa kuwa watanzania watakuwa na uhuru wa kuchagua huduma iliyo bora na manufaa kwao.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema mkongo huo ni mrefu na mkubwa kuliko yote duniani wenye urefu wa kilomita 45,000, unaunganisha watu zaidi ya bilioni tatu katika nchi zaidi ya 33 kwenye mabara ya Afrika, Asia na Ulaya.

Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Rais mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kiwete, alimshukuru Rais Samia kwa kuwafungia mkongo huo chuoni hapo ambao utarahisisha utoaji wa elimu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Airtel nchini, Dinash Balsingh, alisema kwa kupitia ushirikiano unaoendelea kutolewa na serikali wana lengo la kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha uwekezaji wa kidijitali na kuisogeza karibu na dunia.

HABARI KITAIFA

# Korti Kuu yabariki mkataba wa Bandari

**Na Kulwa Mzee,** MBEYA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Mbeya imebainisha kwamba viini vitano kati ya sita vilivyowasilishwa kupinga Mkataba wa Ushirikiano wa Kiuchumi na Kijamii kati ya Tanzania na Dubai (IGA) wa Bandari, havikuwa vinahusu ukiukwaji wa Katiba ya nchi.

Mahakama imesema mkataba huo unaolenga kuendesha, kuwekeza na kuendeleza bandari nchini haukukiuka vifungu vya Katiba ya nchi, hivyo shauri halina mashiko. Linatupiliwa mbali.

Hukumu hiyo ilitolewa jana mbele ya jopo la majaji watatu; Jaji Dunstan Ndunguru ambaye ni kiongozi wa jopo, Jaji Mustafa Ismail na Jaji Abdi Kagomba.

Mwenyekiti wa Jopo, Jaji Ndunguru, alipoanza kusoma hukumu hiyo, alisema raia wa Tanzania wamekuwa wakilalamikia mkataba wa kuwekeza katika Bandari kati ya Tanzania na Dubai. Mkataba huo umekuwa gumzo nchini.

Mkataba huo ulitiwa saini Oktoba 25, 2022 na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa kwa niaba ya Serikali ya Tanzania, baada ya kupewa nguvu ya kisheria na Rais Samia Suluhu Hassan, huku Katibu Mkuu wa wizara hiyo akishuhudia.

Jaji Ndunguru alisema mchakato wa kuridhia ulifanyika, uliwasilishwa bungeni Juni 10 mwaka huu, hatua iliyotanguliwa na taarifa kwa umma iliyotolewa Juni 5 mwaka huu.

Alisema kuwa baada ya Bunge kupitisha kutiwa saini mkataba huo, kulizuka mjadala ukionesha kwamba mkataba una dosari. Haukustahili kuwapo.

Jopo lilisema watu wanne walionesha dosari kubwa katika mkataba huo na katika hati ya madai waliwasilisha misingi minne ya malalamiko yao.

Msingi wa kwanza waleta maombi wanadai kutiwa saini na kuwasilishwa bungeni kwa mkataba huo bila taarifa kwa umma na kutoa muda wa stahiki ni ukiukwaji wa sheria ya mamlaka ya kudumu ya nchi.

Alisema msingi wa pili - mkataba wa IGA uliotiwa saini na mjibu maombi namba mbili na kushuhudiwa na mjibu maombi namba tatu unakiuka sheria na Katiba.

Msingi wa tatu, alisema matendo na mwenendo wa wajibu maombi 2 na 3 waliingiza rasilimali muhimu katika mkataba usio makini.

Katika msingi wanne, walalamikaji wanadai mkataba ulitiwa saini ukiwa na vifungu vinavyohatarisha usalama wa nchi.

"Katika usikilizwaji wa shauri hili, mahakama ilichukua takriban siku tatu. Ilizingatia au kutoa majibu kwa kuangalia viini vikubwa sita," lilisema jopo.

Jaji Ndunguru alitaja kiini cha kwanza endapo utiaji saini, uwasilishaji bungeni na uridhiwaji wa mkataba wa IGA ulikiuka kifungu cha 11(1) na (2) cha Sheria ya Utajiri wa Maliasili Na. 5 wa Mwaka 2017, kikisomwa pamoja na Sheria ya Mapitio na Majadiliano ya Mikataba ya Masharti Hasi, Sheria Na. 6 ya Mwaka 2017.

Kiini cha pili ni endapo umma ulijulishwa na kupewa muda muafaka kushiriki kwenye mjadala na kutoa maoni kwa mujibu wa sheria katika mchakato wa kuridhiwa kwa IGA.

Katika kiini cha tatu ni kama ibara ya 2, 4(2), 5(1),6(2),7(2),8(1)(a)(b)(c),8(2),10(1),20(2)(a), (e)(I) na (Ii),18,21,23(1) na Ibara za 26,27 na 30 za IGA zinakiuka Ibara za 1,8,28(1) na (3) za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kiini cha nne, kama IGA ni mkataba na kiini cha tano kama Ibara ya 2 na 23 ya IGA inakiuka kifungu cha 25 cha Sheria za Mikataba Tanzania.

Alitaja kiini cha sita kama IGA kati ya Tanzania na Dubai ulifuata taratibu za kisheria katika kuchagua njia ya zabuni ambao umewekwa chini ya kifungu cha 64 cha Sheria ya Ununuzi.

"Viini hivyo vililenga kuhoji kama mkataba wa IGA ulikiuka vifungu vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria ya Mikataba, Ununuzi wa Umma na Sheria ya Utajiri wa Maliasili Asilia Na. 5 ya Mwaka 2017, Sheria ya Mapitio na Mijadala ya Vifungu Visivyo vya Haki vya Mikataba ya Utajiri wa Maliasili Asilia ya Mwaka 2017," alisema.

Jaji Ndunguru alisema mahakama ilijielekeza kuangalia iwapo Katiba ilikiukwa ama la, viini vitano kati ya sita havikujielekeza katika ukiukwaji wa Katiba.

"Tunaanza na kiini namba 4 na 5, iwapo IGA ni mkataba na kwamba Dubai haikuwa na hadhi ya kuingia mkataba huo kwa sababu yenyewe si dola.

"Mahakama inakubaliana na hoja za wajibu maombi kwamba mkataba huo lengo lake kuweka msingi wa ushirikiano katika uwekezaji, vifungu vilivyo katika sheria ya mikataba haviwezi kutumika kwa sababu IGA ni mkataba wa kimataifa.

"Hakuna ushahidi kwamba Dubai inazuiwa kuingia katika mkataba, ninakubaliana na wajibu maombi kwamba ilikuwa na hadhi ya kuingia mkataba wa IGA na waleta maombi hawakuleta ushahidi kuonesha Dubai ilikuwa inazuiwa kufanya hivyo.

"Hakukuwa na dosari za kisheria kufanya mkataba wa IGA kuwa batili , mkataba huo ni wa kimataifa, hausimamiwi na sheria za mikataba.

**Katika kiini cha tatu ni kama ibara ya 2, 4(2), 5(1),6(2),7(2),8(1)(a)(b)(c),8(2),10(1),20(2)(a), (e)(I) na (Ii),18,21,23(1) na Ibara za 26,27 na 30 za IGA zinakiuka Ibara za 1,8,28(1) na (3) za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

"Hoja kwamba iwapo mkataba ulikiuka sheria za ununuzi wa umma, mkataba wa IGA haupaswi kusimamiwa na sheria za ununuzi wa umma kwani hakuna ununuzi wa umma uliofanyika kati ya hizo pande mbili.

"Mahakama haijaridhishwa na hoja ya waleta maombi kwa sababu sheria ya ununuzi haiwezi kutumika kupima mkataba wa IGA, " alisema Jaji Ndunguru kwa niaba ya jopo.

Alisema wajibu maombi hawaoni tatizo katika tangazo lililotolewa kwa umma, wanadai vigezo vilitimia na hoja kuwa watu 72 kutoa maoni ni wachache, haina mashiko.

Jaji Ndunguru alisema wajibu maombi walidai kwa kuwa kazi ya wabunge kuwawakilisha wananchi, kitendo cha wao kuridhia mkataba kinatosha kuwawakilisha.

"Njia ya kutoa tangazo katika mtandao ilikuwa sahihi na kwamba kuhusu muda ulikuwa unatosha au hautoshi, mahakama haiwezi kuingilia utendaji kazi wa Bunge," alisema.

Jopo lilisema migogoro ya rasilimali za nchi inapaswa kuamuliwa na mahakama za ndani lakini IGA inataka migogoro iamuliwe na Mabaraza ya Usuluhishi ya Kimataifa.

"Tumebakiwa na mshangao, mikataba itumie sheria za ndani, migogoro itumie sheria za nje lakini Ibara ya 22 ya IGA inatoa nafasi ya kufanya marekebisho ya mkataba huo.

" Hatuoni dosari inayotajwa kuipelekea mahakama kutangaza kuwa mkataba huo ni batili, hatuoni kama hadhi ya nchi imevunjwa.

"Mahakama imebaini na kuhitimisha kuwa Mkataba wa IGA haukukiuka vifungu vya Katiba au sheria mbalimbali.

"Malalamiko kwamba mkataba ulipoka uhuru wa Tanzania kumiliki na kutumia rasilimali asilia bila kuingiliwa na nchi yoyote, hayana mashiko. Yanakataliwa.

"Mahakama haioni kama usalama wa nchi ulikuwa hatarini kutokana na kutiwa saini kwa Mkataba wa IGA. Hatuoni sababu ya kutoa amri ya gharama kwa sababu shauri lina maslahi ya umma," alisema.

Shauri hilo lilifunguliwa na wanasheria watatu kutoka mikoa tofauti; Alphonce Lusako, Emmanuel Chengula, Raphael Ngonde na Mwananchi Frank Nyalus dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Katibu wa Bunge la Tanzania, ambaye ni mtendaji mkuu na mratibu wa shughuli za Bunge.

Walalamikaji wanawakilishwa na Mawakili Mpale Mpoki, Boniface Mwabukusi, Livino Ngalimitumba na Philipo Mwakilima.

Wajibu maombi wanawakilishwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Mark Mlwambo, Wakili Mkuu wa Serikali Edson Mweyunge na Wakili wa Serikali Stanley Kalokola.

Walalamikaji katika shauri hilo wanapinga makubaliano yanayohusu uwekezaji katika bandari za Tanzania zilizoko katika mwambao wa bahari na katika maziwa, kuwa ni batili kwa kuwa yana ibara zinazokiuka sheria na Katiba ya nchi.

Wanadai makubaliano hayo yanahatarisha mamlaka ya nchi na usalama wa Taifa na kwamba yaliridhiwa na Bunge kinyume cha utaratibu bila kuwapa nafasi ya kutosha wananchi kutoa maoni yao.

Kesi hiyo ilianza kusikilizwa Julai 25 mpaka Julai 28 na hukumu kutolewa jana.

**BAADA YA HUKUMU**

Wakili wa walalamikaji, Boniface Mwabukusi, nje ya mahakama alidai hawakuridhishwa na uamuzi huo. Watawasilisha nia ya kukata rufani mara moja.

"Wakati mchakato mwingine wa kisheria unaendelea mahakamani, tunakwenda katika Bunge la wananchi ili liweze kuchukua hatua kulinda rasilimali za nchi.

"Tunaingia barabarani, enzi za kuacha watu wachezee rasilimali na misingi ya Taifa hili zimekwisha, hatutahofu wala hatutaogopa chochote.

"Tunatoa taarifa kwamba sasa ni wakati wa kulinda rasilimali zetu kwa njia za kisiasa kuhakikisha nchi yetu inakuwa salama.

"Mbeya hatutakubali mkataba huu kwa sababu sisi pia ni waathirika. Tuna Ziwa Nyasa. Mahakama imesema haina uwezo kuingilia Bunge. Sasa tutakwenda kutumia Bunge la wananchi, tutatoa siku 14 wasipobadili huu mkataba tutachukua hatua," alidai.

Mwanasheria Lusako ambaye ni mlalamikaji alidai wameshawapa maelekezo mawakili wao kuwasilisha rufani katika Mahakama ya Rufani.

"Tumeona, mmeona jinsi mahakama ilivyopata kigugumizi katika kuamua. Kwa kuwa mahakama hii inaogopa kusema ukweli, basi tutakwenda Mahakama ya Rufani na leo (jana) hiihii tutawasilisha kusudio la kukata rufani," alidai Lusako.

LINDI FORESTS LIMITED

REG: 54989

EXTRACT FROM THE MINUTES OF THE EXTRA - ORDINARY GENERAL MEETING OF LINDI FORESTS LIMITED HELD AT ITS REGISTERED OFFICE

ON 15 JULY 2023 AT 2:00 P.M.

**MEMBERS PRESENT WERE:**

1. GODLISTEN MINJA — **CHAIRMAN** acting representative on behalf of Green Resources AS
2. LILIAN KITOSY — **MEMBER** acting representative on behalf of Nortan AS
3. ANNETTE KIRETHI — COMPANY SECRETARY

**THE CHAIRMAN REPORTED** that according to the Company activities, the Shareholders of **LINDI FORESTS LIMITED** (hereinafter called "the Company") is desirous of voluntarily winding up the Company.

SPECIAL RESOLUTIONS:

**IT WAS RESOLVED.**

1. That, the Company be voluntarily liquidated and dissolved as decided by members;
2. That, Godfrey Basil Mramba be and is hereby appointed as a liquidator for the purpose of winding up the affairs and distributing the assets of the Company;
3. That, the remuneration payable by the Company to shall be negotiated and agreed based on the man-hour spent on this assignment;
4. That **M/S Basil & Alred** be and is hereby appointed auditor for the purpose of auditing the Liquidator's account of the winding up of the affairs of the Company;
5. That the remuneration payable by the Company to **M/S Basil & Alred** as auditor shall be negotiated and agreed based on the man-hour spent on this assignment.

CHAIRMAN

COMPANY SECRETARY

MAZUNGUMZO MAALUM

# Dorothy Semu: Nitawania urais 2025

## - Ataka utaratibu mpya mgawo ruzuku kwa vyama

**Na Waandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa ACT Wazalendo Bara, amesema atawania Urais wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu ujao ikiwa chama hicho kitamteua.

Dorothy Semu, katika mazungumzo maalum na Nipashe katika ofisi za chama hicho mwanzoni mwa juma hili, alisema yuko tayari kupeperusha bendera ya chama hicho katika kinyang'anyiro hicho.

"Mimi ni mwanachama wa ACT Wazalendo, nipo tayari kukitumikia chama kwa lolote lile watakalonielekeza. Kwahiyo, nipo tayari kukitumikia chama."

Dorothy ana sifa za kuwania nafasi ya urais zinazojumuisha umri wa kuanzia miaka 40, kuwa raia wa Tanzania, kuwa mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa.

Mwanasiasa huyo mwenye umri wa miaka 49, ana shahada ya uzamili katika taaluma ya Fiziotherapisti.

Mbali na hoja hiyo ya kuwania urais 2025, katika mazungumzo yake na Nipashe Dorothy pia aligusia mchakato wa katiba mpya na mvutano kati ya chama chake na Chama cha Wananchi (CUF).

Dorothy pia alipendekeza kuanzishwa kwa utaratibu mpya katika utoaji ruzuku kwa vyama vya siasa nchini, ili kila chama chenye usajili wa kudumu kipate ruzuku hiyo badala ya utaratibu wa sasa wa kutoa ruzuku kwa kuzingatia idadi ya wawakilishi bungeni. Ifuatayo ni sehemu ya mazungumzo hayo:



Makamu Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Bara, Dorothy Semu. **PICHA:CARLOS BANDA**

**Swali: Kuna hoja kwamba hakuna usawa kisiasa nchini, ukiwamo ugawaji ruzuku kwa vyama vya siasa. Wewe una mtazamo upi katika hili?**

**Dorothy:** Usawa wa kisiasa hauko vizuri na suala hili haliwezi kuwa na mabadiliko ya haraka kwa sababu chama tawala kina wawakilishi wengi zaidi kulinganisha na vyama pinzani.

Vilevile, suala hili linapelekea hata utoaji wa ruzuku kwa vyama vya siasa kutokuwa na usawa kwa sababu kigezo kikubwa cha kupata ruzuku ni kuwa na wawakilishi wengi kwa wabunge na madiwani.

Ninapendekeza serikali ibadilishe sheria hii na kuweka asilimia 10 kwa kila chama cha siasa nchini kipate ruzuku hizo na kigezo cha wawakilishi kifuate.

**Swali: Serikali imeridhia kufufua mchakato wa katiba mpya. Unafikiri nchi itakuwa na katiba mpya kabla ya 2025?**

**Dorothy:** Mchakato wa katiba ungeendelea na kwa kuwa tunaelekea katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (2024) na Uchaguzi Mkuu (2025), tuwe tayari kufanya marekebisho makubwa kwenye sheria zetu.

Sheria hizo ni za Vyama vya Siasa, Jeshi la Polisi, pia sheria zote zinazogusa uchaguzi, ikiwamo iliyoanzisha Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC). Zipelekwe bungeni na tamko la mchakato wa katiba utaanza lini na kuisha lini litolewe.

Sioni haja ya kuwa na Bunge la Katiba, na tulifikiri serikali itaweka kamati ya wataalamu , ambayo itaangalia maoni yaliyotoka katika Tume ya Jaji (Joseph) Warioba, katiba pendekezwa na maoni mengine yaboreshwe.

Wafanye mapitio hayo na mchakato wa kupiga kura uanze. Hata ikipita katiba mpya leo, itatakiwa kupewa muda ili sheria zipate nafasi ya kuboreshwa ili zilandane na katiba itakayopitishwa.

Mchakato wa kupata katiba mpya ulioanza (mwaka) 2014 uligubikwa na sintofahamu na kuna hoja mbalimbali zisizokuwa na masuluhisho. Sisi tulipata nafasi ya kutoa maoni kwa tume iliyoundwa na Rais Samia Suluhu Hassan kwenye masuala ya demokrasia na tunaona ianze tume huru ili kuelekea mchakato wa katiba mpya.

Tunaamini kupatikana kwa katiba mpya kutaleta uhuru wa kisiasa kwa vyama vya upinzani na chama tawala ili kuleta chachu ya maendeleo ya kidemokrasia na nchi kiujumla.

**Swali: Ni upi msimamo wa ACT Wazalendo katika sakata la Bandari?**

**Dorothy:** Suala la Bandari ni la kisera. Kwa muundo wa uongozi wetu, kiongozi wa Chama ndiye mkuu wa sera na aliunda timu ya wataalamu ndani ya chama na tayari ilifanya kazi yake na ilipewa hadidu za rejea. Timu hii imeshakabidhi ripoti kwa kiongozi wa Chama (Zitto Kabwe).

Ripoti hiyo itakuja kwenye mifumo ya chama kupitia Kamati Kuu, Halmashauri Kuu na kama kutakuwa na Mkutano Mkuu, tutakuwa na tamko rasmi kutoka ndani ya chama kuhusu suala hili.

**Swali: Mmekuwa na mvutano na CUF kuhusu umiliki wa ofisi na mali za chama. Je, mmepata mwafaka?**

**Dorothy:** Kwanza sisi hatuna ugomvi na CUF. Sisi ni chama kinachoamini katika mazungumzo na maridhiano. Ni kweli kulikuwa na changamoto mbalimbali baada ya kushusha tanga na kupandisha tanga.

Pia, changamoto hizo ziliangaliwa kwa jicho la kitaaluma, kitaasisi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alifanya kazi yake kukagua mali na vitu gani ambavyo vilikuwa na visivyokuwa vya CUF.

Alitoa maelekezo kuhusu usajili wa mali na nini kifanyike kuhusu sintofahamu ya mali zilizokuwa za CUF na zile zilizofahamika kuwa za wanachama wa ACT Wazalendo.

**Swali: Unaridhishwa na utekelezaji wa hoja za CAG?**

**Dorothy:** Kwa utawala huu na serikali hali ni ileile. Kwahiyo, huwezi kupata mabadiliko kwa mfumo uliozoeleka kutumika zaidi ya miaka 60.

Ili kupata mabadiliko inabidi kuwa na watu wengi zaidi watakaoweza kuhoji kwa jicho tofauti kwa kuwaingiza viongozi kutoka vyama tofauti katika mfumo na kuleta chachu ya kidemokrasia.

Pia, ripoti ya CAG mara tu inapotolewa, serikali inapaswa kuchukua hatua za haraka juu ya utekelezaji wa masuala mbalimbali yaliyotolewa katika ripoti hiyo kwa usahihi.

**Swali: Unaonaje uongozi wa Rais Hussein Mwinyi na ushiriki wenu katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa?**

**Dorothy:** Sisi ni sehemu ya SUK kutokana na katiba ya Zanzibar, kwamba pale mtu anapopata zaidi ya asilimia 10 (kura za urais) anakuwa sehemu ya umoja huo.

Katika muktadha mbalimbali tumekuwa tukitoa maoni yetu, kwa mambo yanayokwenda vizuri na yasiyoenda vizuri. Tumekuwa tukikosoa na kukemea yanayokwenda vibaya na kutoa njia mbadala ya nini kifanyike.

**Swali: Kipi kimekukosha katika uongozi wa Rais Samia?**

**Dorothy:** Ninaona ni heshima kubwa na ninaamini Rais Samia ameweka historia kubwa inayobadilisha mtazamo katika jamii. Hata mtoto anayezaliwa leo au binti aliyepo shuleni, anaona inawezekana kuwa kiongozi mkuu wa nchi.

Pia, ninaamini yeye kama mama huwa anafanya kazi kwa bidii mno ili aache alama, mabadiliko na ninaamini ndani ya moyo wa Rais Samia hili liko ndani yake.

Kama tunavyoweza kuona, ni Rais ambaye ameweka jitihada, maboresho mbalimbali katika awamu yake ili siku atakayomaliza muda wake tutakuwa na nafasi nzuri ya kumtathimini kuwa alikuta nini na ameacha nini.

Swali: Je, ACT Wazalendo inatilia mkazo usawa wa kijinsia?

Dorothy: Sisi ni chama ambacho tunaamini huwezi kufanikiwa kisiasa bila kumshirikisha mwanamke na kupitia takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, tumeona wanawake ni asilimia 52. Kwahiyo, kumwacha nyuma ni kuacha nusu ya wananchi, nusu ya wapigakura ambao ndio wafanya uamuzi.

Sisi ni chama cha siasa, tuna wanachama wengi wenye uwezo tofauti na jinsi ambavyo wanaweza kuwa gurudumu kubwa litakaloweza kuleta mabadiliko ya kisiasa nchini.

Na hii imekuwa kichocheo cha safari ya kufikia wasemaji wanawake wa kisekta asilimia 54 kwa lengo la kuwainua, kuwawezesha na kuwapa nafasi katika jamii. Hii ni moja ya utekelezaji wa ilani ya chama.

***Imeandaliwa na Mwanahamisi Mussa na Emmaloveness Gaston (TUDARCo)**

# CRDB yajitosa kupunguza bei za simu janja

**Na Mary Seme**

BENKI ya CRDB imeingia ushirikiano na kampuni ya Samsung Tanzania ili kuwapa punguzo la bei wateja wa benki hiyo watakaonunua simu mpya aina ya Galaxy Z Fold5 na Galaxy Z Flip5.

Ushirikiano huo ulitangazwa jana jijini Dar es Salaam na Mkuu wa Huduma za Kadi wa Benki ya CRDB, Farid Seif, aliyeambatana na Mkuu wa Kitengo cha Simu cha Samsung Tanzania, Mgope Kiwanga, mbele ya waandishi wa habari.

Akizungumzia ushirikiano huo, Seif alisema kuanzia sasa, wateja wa benki hiyo wanaopenda kuzinunua simu hizo mpya wanaweza kuweka oda zao ili kuanza kufurahia huduma katika simu hizo zenye ubora wa hali ya juu.

"Katika kipindi hiki, wateja wetu wataokoa kati ya Sh. 308,000 hadi Sh. 565,000 iwapo watanunua simu hizi kipindi hiki cha promosheni.

"Ukienda katika maduka ya Samsung yaliyoenea kote nchini au katika matawi yetu yenye huduma za wateja wakubwa (Premier Banking), utatakiwa kulipia asilimia 20 ya bei ya simu unayoitaka ili kuweka oda na kiasi kilichobaki utakimalizia simu ikishafika.

"Wakati wa kukamilisha malipo ya simu yako utapunguziwa asilimia 10 ya bei ya simu kama utafanya malipo kupitia huduma za malipo za Benki ya CRDB," alisema Seif.

Kwa aliye mbali na duka la Samsung, Seif alisema anaweza kuweka oda yake kwa kuingia katika akaunti za mitandao ya kijamii za Benki ya CRDB katika majukwaa ya Instagram, Twitter na Facebook ambako kuna 'link' itakayowaunganisha na kitengo cha huduma kwa wateja cha Samsung Tanzania ambako wanaweza kuweka oda ya simu waitakayo.

"Kwa njia yoyote kati ya hizi, mteja atakayelipa kwa kutumia kadi ya Benki ya CRDB au kupitia SimBanking atarudishiwa asilimia 10 ya malipo aliyoyafanya," alisisitiza Seif.

Kwa miaka mingi, Benki ya CRDB imekuwa inaongoza kwa ubunifu katika kutoa huduma wateja wake. Ilikuwa ya kwanza kuanzisha matumizi ya kadi zinazofahamika zaidi kama CRDB Bank TemboCard na ikawa ya kwanza kuzindua programu ya huduma kupitia simu za mkononi almaarufu kama SimBanking ambayo inaongoza kwa kutumiwa nchini miongoni mwa programu za benki zilizopo.

Kwa Watanzania ambao hawajajiunga na huduma za Benki ya CRDB, hivyo kutokidhi vigezo vya kunufaika na punguzo hili, Seif alisema wanakaribishwa kufanya hivyo na kuwa sehemu ya mtandao mkubwa wa matawi yaliyoko katika wilaya zote nchini na huduma za mawakala wengi wanaopatikana mitaani kote.

"Kwa sasa utaratibu umerahisishwa, mteja anaweza kujifungulia akaunti yeye mwenyewe au akaenda kufungua kwa wakala yaani CRDB Bank Wakala au akaenda katika tawi letu lolote na kuanza kufurahia huduma likiwamo punguzo la bei la simu bora za Samsung," alisema Seif.

Kuhusu unafuu uliopo, Kiwanga alisema mteja atakayenunua simu zinazoingizwa sokoni kwa sasa atanufaika na punguzo hilo la bei, na atapata saa ya mkononi yenye thamani ya Sh. 900,000 au 'earpods' zinazouzwa Sh. 450,000 kutegemeana na aina ya simu atakayoinunua.

"Simu aina ya Galaxy Z Fold5 tunaiuza kwa Sh. milioni 5.65 na ile ya Galaxy Z Flip5 ni Sh. milioni 3.08. Ukiweka punguzo la asilimia 10 ambalo mteja atalipata akilipa kupitia mifumo ya Benki ya CRDB pamoja na zawadi hizi anazopewa, utaona kuwa anaipata simu hii kwa bei ndogo kuliko uhalisia wake.

"Ninawakaribisha Watanzania kuchangamkia fursa hii katika maduka yetu ndani ya kipindi cha promosheni kitakachodumu mpaka mwishoni mwa mwezi huu," alisema Kiwanga.



Vijana wakitoa mchanga ulioziba mifereji ya kupitisha maji ya mvua katika mtaa wa Sokoine, mjini Babati mkoani Manyara jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Adaiwa kumuua mama yake kwa mchi hatimaye kumbaka

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKAZI wa Ludewa mkoani Njombe, Asifiwe Haule (25), anashikiliwa na Jeshi la Polisi wilayani humo kwa madai ya kumuua mama yake mzazi, Ubatizo Sanga (55) kwa mchi hadi kufa kisha kumbaka.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Victoria Mwanziva, alisema tukio la mauaji ya mama huyo ambaye ni muuguzi za zahanati ya mawengi wilayani humo, lilitokea Agosti 8, mwaka huu, majira ya saa 10:00 jioni kijijini Mawengi.

"Nimetoka kuongea na Kaimu OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya) ameniambia tukio hilo kwa kina na huyo mhusika tayari yuko chini ya ulinzi na usalama unaendelea kuimarishwa kwani tukio limetokea ndani ya familia husika.

Mtu mkubwa kama huyu angekua hajakamatwa ina maana ingeweza kuleta shida kwenye jamii lakini ni mhalifu ambaye amekwisha kukamatwa," alisema. Mwenyekiti wa kijiji cha Mawengi, Renatho Kahako, alisema mtoto huyo alifanya mauaji na baadaye alibaka maiti.

"Huyu kijana ni kama alikua amechanganyikiwa. Muda mrefu kidogo alikuwa hayuko timamu," alisema Kahako.

Diwani wa Mawengi, Leodgar Mpambalyoto, alisema muuguzi huyo alikuwa akiishi na mtoto wake huyo kwa muda mrefu.

"Ni kweli japo mimi sikuwapo, alikuwa akiishi na kijana wake. Sasa hatujui ilikuwaje hadi achukue uamuzi huo," alisema. Mmoja wa majirani ambaye hakutaka jina lake litajwe gazetini, alisema jambo hilo ni baya kutokea katika eneo hilo licha ya mtoto huyo kuwa na migogoro ya mara kwa mara na mama yake.

# ACT-Wazalendo yapongeza vikao kamati maridhiano ya kisiasa kuleta matumaini

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema kuanza kwa vikao vya Kamati ya pamoja ya maridhiano ya kisiasa kati ya Chama cha ACT -Wazalendo na Chama Cha Mapinduzi (CCM), ni hatua muhimu ya kutia moyo na ya kuleta matumaini ya kuwapo na kuendeleza mjadala wa masuala mbalimbali yanayohusu mustakabali mwema wa Zanzibar.

Othman alisema hayo nyumbani kwake Chukwani, alipokutana na Balozi mdogo wa Uingereza nchini Tanzania, Rick Shearn, aliyetaka kujua pamoja na mambo mengine ya maendeleo ya kamati hiyo ya pamoja iliyoundwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Alisema hivi sasa kamati hiyo imeanza vikao vyake kwa kujadili maeneo na agenda muhimu na mahususi na namna ya utaratibu bora utakaotumika katika kuyajadili masuala muhimu kwenye agenda hizo ili kufikia muafaka kwa malengo yaliyokusudiwa ya mustakabali wa Zanzibar na watu wake.

Pia, alisema anaamini kwamba katika vikao hivyo vya awali maeneo yote muhimu yanayohitaji kufanyiwa mabadiliko na mageuzi makubwa yameainishwa kwa kuwasilishwa na kujadiliwa kwa pamoja katika kutafuta maslahi bora ya Zanzibar na watu wake.

Alisema, kuwapo kwa hatua hiyo ni fursa muhimu kwa Zanzibar katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi wa 2025 kufanya mabadiliko na mageuzi yanayotarajiwa na wananchi wa Zanzibar katika kuweka matumani ya mustakabali wa nchi yao. Kadhalika, alisema majadiliano hayo ya awali yamegusa maeneo muhimu yote likiwamo suala la Mageuzi na mabadiliko katika masuala ya uchaguzi ikiwamo Tume inayosimamia uchaguzi ili kuifanya kuwa taasisi imara kwa maendeleo na mustakabali mwema wa Zanzibar.

Alisema kwamba agenda ya mausuala ya uchaguzi inaendelea kama jambo muhimu katika misingi ya mjadala huo kwa kuwa unalenga maisha ya Wazanzibar, biashara kwa Zanzibar, pia ni uwekezaji kwa maendeleo ya nchi.

Zanzibar alisema inahitaji uwekezaji na wawekezaji wanahitaji kuwekeza fedha zao katika eneo salama na lenye utulivu ili waweze kufanya biashara na wageni kutembea Zanzibar kupitia sekta ya utalii.

Masuala mengi yanagusa mambo muhimu ikiwamo pia mabadiliko katika sekta za umma na kuwapo uwajibikaji na utawala wa sheria yameainishwa kwa kuwa ni mambo yatakayosaidia kuondoa udhaifu katika maeneo mbali mbali ya sekta za umma ili kujenga maendeleo endelevu ya Zanzibar.

Akizungunzia suala la Katiba mpya, Othman alisema kwamba hilo ni suala la Muungano, lakini linagusa maendeleo ya masuala kadhaa ya Zanzibar moja kwa moja na mengi yanayohitaji kufanyiwa mageuzi katika usimamizi na uendeshaji wake ikiwamo haki jinai na uchaguzi wa wabunge na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Balozi Shearn alitaka kufahamu iwapo suala la Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pia linaweza kuathiri mustakabali wa Zanzibar katika uchaguzi ujao wa 2025 na utekelezaji wa msuala mbali mbali ikiwamo uchaguzi wa Zanzibar.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Neema ya matibabu nyonga, magoti ilenge waliokusudiwa

**NEEMA** ya matibabu ghali imeendelea kuishukia Tanzania baada ya kutangazwa kwa ujio wa madaktari bingwa 60 wa mifupa kutoka Marekani ambao wataweka kambi ya siku saba katika Hospitali ya Seliani, mkoani Arusha.

Madaktari bingwa hao ni wageni maalumu wa Rais Samia Suluhu Hassan na watatoa huduma ya upasuaji bure kwa wenye matatizo ya nyonga na magoti kwa watu kutoka familia zisizo na uwezo kuanzia leo.

Wataalamu hao wa mifupa wanaingia nchini kufanya huduma kwa kuitikia wito wa Rais Samia alioutoa alipofanya ziara nchini Marekani hivi karibuni. Pia ujio wao ni katika kuendeleza uhusiano wa muda mrefu kati ya Marekani na Tanzania uliojengwa baina ya mataifa hayo na wadau wengine kutokana na nafasi zao.

Ni wazi kwamba Watanzania wengi hawana uwezo wa kumudu gharama za matibabu makubwa kama ya upasuaji wa viungo vya mwili, hivyo kuwapo kwa huduma hiyo ni neema kwa wananchi wenye uhitaji huo. Kwa kawaida, matibabu ya upasuaji wa nyonga na magoti kwa mtu mmoja yanagharimu Dola za Marekani 30,000 sawa na Sh. Milioni 70 za Kitanzania, hivyo walengwa kutoka katika familia zisizojiweza hawana budi kuchangamkia fursa hiyo.

Licha ya kwamba ni fursa kwa Watanzania, jopo hilo la madaktari na huduma watakayoitoa, zitaifanya Hopitali ya Seliani itakayokuwa mwenyeji wa matibabu hayo kujenga jina ndani na nje ya mipaka pamoja na shughuli hiyo kutumika kama sehemu ya taasisi kuongeza viwango kwa kutoa matibabu ya kibingwa. Kwa maneno mengine, huduma hiyo itakuwa sehemu ya madaktari wazawa katika hospitali hiyo kupata maarifa ya utoaji huduma kutoka kwa madaktari wabobezi kutoka Marekani.

Hii si mara ya kwanza kwa madaktari bingwa kutoka nje ya nchi kuja kutoa huduma za upasuaji ambazo zinahitaji umakini na umahiri mkubwa. Tanzania imeshuhudia madaktari kutoka nchi mbalimbali kama vile India na China ambao wamekuwa wakiingia nchini mara kwa mara kufanya upasuaji wa viongo vya binadamu kwa kushirikiana na madaktari wazawa kwa hiyo fursa hii inatoa nafasi kwa wagonjwa wenye uhitaji wa huduma hiyo.


Hata hivyo, Habari njema ni kwamba tayari wagonjwa wameanza kumiminika kujiandikisha kwa ajili ya kupata huduma hiyo. Wakati taarifa ya ujio wa madaktari hao ikitolewa, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Seliani, Dk. Goodwill Kivuyo, alisema hadi Jumatatu wiki hii, zaidi ya wagonjwa 200 walikuwa wamejiandikisha kwa ajili ya huduma hiyo.

Pamoja na mkurugenzi huyo kuweka bayana kwamba watakaonufaika na matibabu hayo ni wale wanaotoka familia zisizojiweza, ujanja usipewe nafasi kwa watu wenye uwezo kuchomekwa na kupatiwa matibabu huku waliokusudiwa wakikosa huduma hiyo. Tunasema hivyo kwa sababu kumekuwa na matukio mbalimbali kwa watu waliopewa dhamana kuwaingiza hata ndugu zao katika huduma fulani na kuwaacha walengwa.

Ni vyema viongozi waliopewa dhamana ya kusimamia jambo hilo wakafanya kazi kwa weledi kwa kuhakikisha wanaopata huduma hiyo ya matibabu ya kibingwa ni wale waliokusudiwa na si vinginevyo. Viongozi hao wanapaswa kutojiingiza katika vitendo vya aibu kama vile rushwa kwa kupokea fedha kutoka kwa wenye ukwasi ili watu wao wapendelewe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Napiga makofi mapinduzi ya dijitali ila tuwe macho wanakoelekea vijana

Na Ester Mbilinyi, TUDARCo

**UKUAJI** wa teknolojia duniani umebadilisha mambo mengi duniani, ikiwa ni pamoja na namna watu wanavyowasiliana.

Mawasiliano kati ya mtu na mtu kwa sasa yapo kiganjani ikilinganishwa na miaka ya 1990 kurudi nyuma, wengi waliwasiliana kwa barua kwenda kwa bibi kijijini, ambayo ilimfikia mhusika ikiwa imechelewa.

Umuhimu wa teknolojia unadhihirishwa na tukio lililofanyika jana la Rais Samia Suluhu Hassan, kuzindua mkongo mkubwa wa mawasiliano, unaopita baharini, pia akazindua teknolojia ya mawasiliano ya masafa ya juu ya kampuni Airtel 5G.

Ukuaji teknolojia, umerahisisha mambo. Badala ya mtu kutumia mlolongo mrefu kufikisha ujumbe kwa ndugu na jamaa, sasa anapokea ujumbe kwa sekunde kwa kupiga simu bila ya kujali umbali. Na hii ndiyo maana ya dunia ni kijiji.

Hivi karibuni kumekuwapo na wimbi kubwa la watumiaji wa simu janja. Yote ni zao la kasi ya kukua teknolojia. Wapo wanaozitumia simu kufanya makubwa, hata kubadilisha maisha katika kipato.

Wanatumia majukwaa kutangaza biashara maarufu 'biashara mtandao' sasa nchi mbalimbali zinatumia teknolojia kufikishia ujumbe haraka kwa wateja wao.

Mashirika na kampuni zinafikia malengo kwa kipindi kifupi, kupitia matumizi ya sahihi ya teknolojia, simu janja ikirahisisha.

Mfanyabiashara wa nguo, Emmanuel Gavile, anasifu namna simu janja inavyomrahisishia kumuunganisha na wateja wao mikoa tofauti, badala ya kutumia majukwaa mitandaoni kujitangaza.

Mwanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Tumaini (TUDARCo), Asma Hassan, anaelezea umuhimu mkubwa wa simu janja katika masomo yake, yanamwezesha kupata taarifa za chuo na kumfanya asibaki nyuma kimasomo darasani.

Kwa wakulima vijijini, simu imekuwa kiunganishi wa masoko yao, wapo waliojiunga katika makundi mitandaoni na imewarahisishia kulima kisasa, hata kupata soko la uhakika.

Kwa upande mwingine itakapotumiwa vinginevyo, ni janga hasa kwa vijana ambao kwa kiwango kikubwa wamekuwa wakishinda mitandaoni.

Athari hizo ni pale zisipodhibitiwa vema, endapo zitadhibitiwa kuna umuhimu katika maisha kwa kumkomboa katika suala la kupata ajira.

Pia, kuna mambo mengine yasiyoendana na utamaduni wa Mwafrika, ambayo kushinda kwao mitandaoni vijana, wamekuwa wakiangalia picha na video zisizofaa, hata leo viongozi mbalimbali wanasimama kwenye majukwaa wakizungumzia mmomonyoko mkubwa wa maadili kwetu vijana.

Tumekuwa tunaiga utamaduni wa mbali, ikiwamo uvaaji na sasa kunashuhudiwa vijana wa kiume wakivaa suruali zikiwa zimeshuka mapajani maarufu 'mlegezo' na mabinti wakivaa nguo zisizositiri miili yao kama kuonyesha tumbo, matiti na kitovu na wengine wakiiga vitendo vingine kinyume na Mwafrika alivyo.

Matumizi yasiyofaa, pia yamechangia jamii badala ya kuishi kwa amani na upendo, sasa kuna matukio ya mauaji yakiwamo yanayotajwa 'wivu wa mapenzi kwa wanandoa' yakisababishwa na simu.

Kumekuwapo na ongezeko la ugomvi kwenye uhusiano au ndoa kwa baadhi ya wanawake kushindwa kutimiza majukumu yao kwa wenza wao, kwa kutumia muda mwingi kushinda mitandaoni.

Vilevile kutokana na kutokuwa na elimu isiyofaa kwa matumizi ya simu, baadhi ya watu wanapiga picha zisizofaa au kurekodi video chafu na kuzitupia mitandaoni kinyume cha utamaduni wa Waafrika.

Kutokana na ukuaji huu wa teknolojia ni lazima kila mmoja kuhakikisha anaitumia simu kwa manufaa chanya kwa kujiletea maendeleo binafsi, jamii na taifa kwa ujumla.

Ili kujiepusha kizazi kijacho kuingia kwenye janga kubwa la mmomonyoko wa maadili, wazazi wahakikishe hawawamilikishi simu watoto wakiwa kwenye umri mdogo, ambao bado hajawajitambua.

Tunahitaji makundi mbalimbali yanayokemea vitendo visivyofaa vinavyochangiwa na kasi ya ukuaji wa teknolojia, vijikite kuelimisha jamii namna bora ya kumfanya kijana aweze kunufaika na simu janja kwa kubadilisha maisha yake na kuleta chachu ya maendeleo kwa taifa.

## HABARI KITAIFA




Mkurugenzi wa Hazina wa Benki ya Azania, Gilbert Mwandimila (wa pili kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Agricom Africa, Alex Duffar (wa pili kulia), wakitiliana saini mkataba wa makubaliano wenye lengo la kumwezesha mkulima kupata zana bora za kilimo kupitia mkopo wa masharti nafuu, katika maonyesho ya wakulima Nanenane, jijini Mbeya juzi. Wengine ni Mkuu wa Idara ya Kilimo wa benki hiyo, Augustino Matutu (kushoto) na Meneja wa Agricom tawi la Kanda ya Kusini, Joseph Manoni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kamati ya Bunge kupokea maoni Muswada wa Sheria ya Ununuzi

**Na Maria Semi**

KAMATI ya Bunge ya Bajeti inatarajia kuanza kupokea na kusikiliza maoni ya wadau kuhusu muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa mwaka 2023, unaolenga kuondoa vikwazo mbalimbali vilivyobainika kwenye eneo la ununuzi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Ofisi ya Bunge, Kamati hiyo itaanza kupokea maoni hayo Agosti 15 na 16, 2023 katika Ukumbi wa Pius Msekwa, Ofisi ya Bunge, jijini Dodoma.

Muswada huo unapendekeza kutunga upya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023 kwa lengo la kuweka masharti bora ya usimamizi wa ununuzi wa umma na ugavi.

Sheria inayopendekezwa inakusudia kutatua vikwazo vilivyobainika katika utekelezaji wa masharti na taratibu za ununuzi na ugavi.

Miongoni mwa vikwazo ni pamoja na muda mrefu wa hatua za ununuzi, bei kubwa ya bidhaa, huduma na kandarasi ikilinganishwa na bei halisi ya soko, kutojumuishwa kwa masuala ya usimamizi wa ugavi katika sheria hiyo na kukosekana kwa masharti yanayoruhusu kuwapo utaratibu mahsusi wa ununuzi kwa taasisi za umma zinazojiendesha kibiashara.

Sheria inayopendekezwa kutungwa inajumuisha masharti yatakayowezesha ununuzi, ugavi na uondoshaji mali kufanyika kwa wakati na kwa kuzingatia uadilifu, uwajibikaji na usawa ili kuwezesha upatikanaji wa thamani ya fedha.

Aidha, ili kuhakikisha uwazi katika hatua zote za ununuzi na ugavi, sheria inayopendekezwa inaweka masharti ya lazima kwa shughuli zote za ununuzi na ugavi kufanyika kupitia mfumo wa kielektroniki, ili kuhakikisha uwazi katika mchakato wa ununuzi na kuondoa ucheleweshaji unaoweza kuepukika katika hatua mbalimbali za ununuzi na ugavi.

Sheria inayopendekezwa itatumika katika hatua zote za ununuzi, ugavi na uondoshaji mali kwa njia ya zabuni unaogharamiwa kwa fedha za umma na kuweka masharti kuhusu misingi na viwango vya kuzingatiwa katika ununuzi, ugavi na uondoshaji mali na miongoni mwa misingi hiyo ni kuhakikisha fursa na haki sawa kwa wazabuni, uendelezaji wa viwanda vya ndani na umuhimu wa kupata thamani ya fedha katika bei, ubora na huduma zinazotolewa.

Aidha, Mamlaka ya Udhibiti Ununuzi wa Umma itakuwa pia na jukumu la kuandaa na kutunza taarifa kuhusu bei kikomo kwa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma zinazogharamiwa kwa fedha za serikali, ili kuhakikisha upatikanaji wa thamani ya fedha na kwamba bei husika zinaendana na bei halisi ya soko.

Aidha, unapendekeza masharti yanayoelekeza kuwa Vitengo vya Usimamizi wa Ununuzi na Ugavi vitakuwa na wataalamu wa ununuzi na ugavi wenye sifa stahikii za kitaaluma.

Kadhalika Muswada unahusu masharti ya usimamizi wa mikataba ya zabuni na ofisa masuuli ana wajibu wa jumla katika utekelezaji wa mkataba wa zabuni.

Muswada unaweka masharti kuhusu vitendo na mienendo mbalimbali inayokatazwa katika mchakato wa ununuzi ikiwamo rushwa, udanganyifu, ulaji wa njama na ushawishi katika mchakato wa ununuzi au utekelezaji wa mkataba unaogharamiwa kwa fedha za umma.

## CPA yakutana Dar kujadili mfumo mpya

**Na Elizabeth Zaya**

KAMATI ya Utendaji ya Mabunge ya Jumuiya ya Madola (CPA), tawi la Afrika, imekutana Dar es Salaam kujadili namna ya kubadili mfumo wa uendeshaji kutoka kuwa ya msaada kwenda kwenye uamuzi.

Kamati hiyo ikiongozwa na Mwenyekiti, Catherine Hara, ilikutana kwa siku moja juzi Dar es Salaam.

Naibu Spika, Mussa Zungu, alisema kwa sasa vikao vyote vya CPA vinachukuliwa kama chombo cha msaada na lengo ni kubadili kanuni zake za uendeshaji ili kiwe cha uamuzi na kimataifa zaidi.

"Tunataka kiwe ni chombo ambacho kitakuwa na maamuzi ambayo yatapelekwa Umoja wa Mataifa na yatekelezwe na mabunge ya nchi ambazo ni wanachama wa CPA," alisema Zungu.

"Kwa hiyo kikao hiki cha utendaji kimekaa hapa kuweka mikakati ya mkutano ambao utafanyika Septemba Accra-Ghana wa kuwa na msimamo wa pamoja wa kubadilisha mfumo huo na kukitambua kuwa ni cha kimataifa na kinakuwa na mamlaka ya kisheria ya kudhibiti au kuwa na uwezo wa kusaidia nchi zingine kufanya uamuzi wake."

Pia, alisema kikao hicho kilijadili mambo mengine, ikiwamo yanayohusiana na uchumi kwa nchi za Afrika pamoja na masuala ya kimataifa.

Mwenyekiti wa CPA, Catherine, alisema mambo mengine waliyojadili katika kikao hicho ni namma ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika vyombo vya uamuzi.

"Agenda yetu kubwa ni kutaka kubadili mfumo wa kiuendeshaji wa chombo hiki kuwa wa kimataifa zaidi kuliko ulivyo hivi sasa, kuangalia mambo yenye mustakabali wa CPA ambayo tumekuwa tukiyajadili kwa muda mrefu ili tufikie muafaka pamoja na kuangalia namna ya kuongeza idadi ya wanawake kwenye vyombo vya uamuzi," alisema Catherine.

"Kabla ya mkutano wa kimataifa utakaofanyika Accra-Ghana, sisi kama nchi za Afrika tunatakiwa tukae chini tujadili na kuangalia uwezekano ambao utatupeleka mbele zaidi tutakapokwenda huko.

Pia tutaangalia namna nchi zetu zinavyojiendesha."


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,

........Tarehe...10/08/2023

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMAMOSI tarehe 12/08/2023 kampuni ya Transcargo Ltd itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka DAR ES SALAAM kuelekea RUSUMO, gari hilo lenye namba za usajili:
T 799 CPQ/T 201 EAZ
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
Urefu - mita 20
Upana - mita 4.3
Kimo - mita 4.8
3. Njia itakayotumika: DAR ES SALAAM hadi RUSUMO Kupitia MOROGORO, gari litasafiri muda wa mchana tu (**Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni**)

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

Transcargo Ltd OPERATIONS @ TRANSCARGO CO. LTD 10 AUG 2023 OPERATIONS DEPARTMENT

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,

........Tarehe...10/08/2022

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMAMOSI tarehe 12/08/2023 kampuni ya TRANSCARGO LTD itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka DAR ES SALAAM kuelekea RUSUMO, gari hilo lenye namba za usajili:
T 646 EAE/T 583 DFL
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
Urefu - mita 22
Upana - mita 4.3
Kimo - mita 4.8
3. Njia itakayotumika: DAR ES SALAAM hadi RUSUMO Kupitia MOROGORO, gari litasafiri muda wa mchana tu (**Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni**)

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

Transcargo Ltd OPERATIONS @ TRANSCARGO CO. LTD 10 AUG 2023 OPERATIONS DEPARTMENT

# Kiwanda cha kwanza cha vioo kuanza uzalishaji nchini Septemba

**Na Joseph Mwendapole**

KIWANDA cha kwanza cha aina yake kujengwa nchini cha kutengeneza vioo cha Sapphire Glass, kinatarajia kuanza uzalishaji mwezi ujao na kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 250,000 kwa mwaka.

Ujenzi wake umegharimu Sh. bilioni 750 ni cha nne kujengwa Afrika cha kwanza kikiwa nchini Afrika Kusini, viwili nchini Nigeria na Sapphire Glass cha Tanzania kitakuwa cha nne.

Hayo yalisemwa jana kiwandani hapo Mkuranga mkoa wa Pwani na Mkurugenzi Mkuu wa kiwanda hicho, Jack Feng, wakati wa ziara ya Waziri wa Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo.

Alisema uzalishaji wa kiwanda hicho utakidhi mahitaji ya vioo kwa hapa nchini na kwamba mauzo ya ndani yatakuwa asilimia 25 pekee wakati mauzo ya nje ya nchi ni asilimia 75.

Alisema kiasi kikubwa cha vioo kitauzwa kwenye nchi za Jumuiya ya Kusini mwa Afrika (SADC), Afrika Mashariki na nchi jirani zenye mahitaji ya bidhaa hiyo.

Naye Waziri Mkumbo alisema kiwanda hicho kitakuwa cha nne kwa Afrika, cha kwanza kikiwa Afrika Kusini, viwili nchini Nigeria na Sapphire Glass cha Tanzania kitakuwa cha nne.

"Huu ni uwekezaji mkubwa sana kwasababu ujenzi pekee wa kiwanda umegharimu Dola za Marekani milioni 301 ambazo ni sawa na Sh. bilioni 750 na sisi kazi yetu ni kuvutia mitaji mikubwa kama hii kama mnavyoona huu siyo uwekezaji wa kawaida," alisema na kuongeza

"Pili tunavutia teknolojia ukiangalia hii teknolojia hatuna kwa sasa wanayo Afrika Kusini na Nigeria na tunataka kuongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi kwa hiyo tutaungana na nchi ambazo zinauza vioo nje ya nchi," alisema.

Aidha, Waziri Mkumbo alisema kiwanda hicho kitazalisha ajira za moja kwa moja 1,600 na 6,000 zisizo za moja kwa moja na malighafi za uzalishaji zitatoka nchini.

Alisema, anafurahi kuona malengo yote manne ya serikali yanakamilika ambayo ni kuvutia uwekezaji, kuvutia teknolojia, kuongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi na kutengeneza ajira.

Alisema kiwanda cha Sapphire kilianza kujengwa Julai mwaka jana na mwaka huu wanatarajia kuanza uzalishaji ifikapo Septemba na kwamba hayo yote yanafanyika kutokana na sera nzuri za uwekezaji za serikali ya awamu ya sita.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji (TIC), Gilead Teri, alisema uwekezaji huo ni wa kimkakati ambao wamesajiliwa kwenye kituo hicho na wamewapa vivutio mbalimbali vya kuwawezesha kupunguza gharama za mitaji yao.

"Wanapoingiza mashine na mitambo ya uzalishaji serikali imeweka sheria ambayo inawaondolea asilimia 75 ya kodi ya uingizwaji wa bidhaa nchini import duty na hiyo inasadia kuifanya Tanzania kuwa sehemu salama na nzuri kwa wawekezaji," alisema Teri.

Alisema TIC imeanzisha mifumo mbalimbali ya kielektroniki ikiwemo dirisha la pamoja kwa ajili ya kuwahudumia wawekezaji na kuongeza maboresho ya huduma zinazotolewa na kituo hicho kwa kanda mbalimbali nchini.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (kushoto) akiagana na Mkurugenzi Mwenza wa kampuni ya Franone Mining and Gems Ltd, Francis Matunda, inayochimba madini ya Tanzanite eneo la kitalu C mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro, baada ya kutembelea eneo hilo juzi. **PICHA GIFT THADEY**

# 'Miradi ya Tehama iwasilishwe e-GA'

**Na Mary Seme**

MAMLAKA ya Serikali Mtandao (e-GA), imeziagiza taasisi za umma kuwa miradi na mifumo yote ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) inayotekelezwa ndani ya taasisi zao inawasilishwa e-GA wakati wa hatua ya mipango ili kuiwezesha mamlaka kupitia na kutoa ushauri wa kitaalamu kabla ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Agizo hilo limetolewa jana na Meneja wa Usimamizi wa Udhibiti na Viwango vya Serikali Mtandao, Sultana Seiff, wakati wa kufunga mafunzo ya siku mbili kwa maofisa TEHAMA na Rasilimali watu kutoka katika taasisi mbalimbali za umma zilizo katika sekta ya uchukuzi yaliyofanyika mkoani Morogoro, kuanzia Agosti 9, mwaka huu.

Alisema, agizo hilo ni utekelezaji wa matakwa ya kifungu Na. 24 cha Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019 pamoja na Kanuni Na.27 ya Kanuni za Jumla za Serikali Mtandao za mwaka 2020.

"Taasisi zote za umma zinapaswa kuwasilisha taarifa kamili na sahihi za miradi na mifumo yote ya TEHAMA kupitia Tovuti ya Huduma za TEHAMA serikalini ijulikanayo kama 'Government ICT Service Portal (GISP)' ili e-GA ifanye mapitio ya miradi hiyo na kutoa ushauri wa kitaalamu pamoja na kibali," alisema Sultana.

Alifafanua kuwa pamoja na uwapo wa sheria hiyo, mamlaka imeandaa viwango na miongozo ya serikali mtandao ambayo taasisi zote za umma zinapaswa kuzingatia katika usimamizi na utekelezaji wa miradi, mifumo na miundombinu ya TEHAMA ili kuhakikisha kuwa jitihada hizo zinakua ni salama, sahihi, bora, endelevu na zenye kuzingatia thamani halisi ya pesa. Lengo la Mamlaka ya Serikali Mtandao ni kuhakikisha taasisi za umma zinatumia TEHAMA katika utendaji kazi wake na utoaji wa huduma kwa wananchi ili huduma hizo zipatikane kwa wananchi wote kwa wakati mahali walipo na kwa gharama nafuu, alisema.

Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi katika Sekta ya Uchukuzi, Leonard Lwiza, alisema ufanisi wa utendaji kazi katika sekta ya uchukuzi unategemea ujenzi na kuwapo mifumo salama na imara ya TEHAMA na ni muhimu mifumo hiyo izingatie sheria, kanuni, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao. Aidha, aliwataka maofisa TEHAMA walioshiriki mafunzo hayo, kuwa mawakala wazuri kwa kuhakikisha miradi na mifumo yote ya TEHAMA katika taasisi zao inazingatia sheria, kanuni, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao.

Ofisa Rasilimali watu kutoka Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Bakari Mbaga, alishukuru e-GA kwa kuandaa mafunzo hayo ambayo yamewajengea uwezo kuhusu sheria, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao na umuhimu wake katika kuhakikisha taasisi za umma zinatumia vema TEHAMA ili kuimarisha jitihada za Serikali Mtandao.

# Utafiti wabaini mbinu kuepuka magonjwa ya moyo

**Na Maulid Mmbaga**

WATAFITI wa Chuo Kikuu cha Tiba Johns Hopkins cha Marekani na Chuo Kikuu cha Lodz Poland, wamebaini kutembea hatua 5,000 kwa siku kunatosha kuimarisha afya ya binadamu, ikiwamo kuepukana na magonjwa ya moyo.

Utafiti wa awali ulishauri mtu kutembea hatua 10,000 kila siku ili kuepuka matatizo ya kiafya yakiwamo ya moyo, lakini utafiti mpya umegundua kuwa hata wasioweza kufikisha hatua 5,000 wanapomudu 4,000 zinatosha kumuepusha kuwa katika hatari ya kufariki dunia kutokana na magonjwa ya moyo.

Kwa mujibu wa utafiti huo uliotolewa siku chache zilizopita, unaotajwa kuhusisha zaidi ya watu 200,000 watafiti wamegundua kuwa manufaa ya kutembea kila siku yanawahusu watu wa tabaka zote bila ya kujali jinsia, umri au wanakoishi. Na kwamba wanaonufaika zaidi ni watu walio chini ya umri wa miaka 60.

"Kila hatua 1,000 zaidi ya hizo 4,000 zinapunguza hatari ya kufa mapema kwa hadi asilimia 15," alisema.

Mratibu wa Magonjwa Yasiyoambukiza (NCD), Dk. Milka Mathania wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, ameiasa jamii kufanya mazoezi ambayo kimsingi hulinda afya zao dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza (NCDs), huku akibainisha kwamba magonjwa hayo yanaitesa jamii.

"Ongezeko la watu wenye magonjwa yasiyoambukiza ni changamoto kwa taifa na dunia kiujumla ambayo husababishwa na aina ya maisha ya watu na chakula huku suala la mazoezi likiwekwa kando," alisema.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), kutofanya mazoezi ya kutosha, ni chanzo cha nne cha vifo vingi zaidi ulimwenguni. Na kwamba takribani watu milioni 3.2 hufariki dunia kila mwaka kwa kukosa mazoezi ya kutosha ya viungo.

Pia, wataaalamu wanaonya kuwa kukaa chini kwa muda mrefu kuna sababisha athari nyingi ikiwamo matatizo ya mgongo hasa kwa wanafanya kazi za ofisini ambao mara nyingi hukaa kwa kujipinda kwa muda mrefu na hata kama siyo mara moja, baadaye maishani, hukumbwa na matatizo ya uti wa mgongo na shingo.

"Kutembea kuna punguza shinikizo la damu, linaimarisha afya ya misuli na mifupa, inampa mtu nguvu zaidi kwa kuongeza viwango vya homoni ya endorphine na inasaidia katika kudhibiti uzito wa mwili. Manufaa mengine ni inaimarisha afya ya akili na kumpa mtu fursa ya kufanya shughuli nyingine za kila siku," ilisema WHO.



# CCBRT yatoa msaada viti mwendo shule za msingi, awali

**Na Allan Isack,** ARUMERU

WANAFUNZI 17 wenye ulemavu wa viungo katika shule za msingi na awali katika Halmashauri ya Arusha wilayani Arumeru, wamepatiwa msaada wa viti mwendo 17.

Msaada huo umetolewa na Hospitali ya CCBRT Kanda ya Moshi na kukabidhiwa kwa uongozi wa halmashauri hiyo kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi hao.

Akizungumza jana wakati wa kukabidhi kwa viti mwendo hivyo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Arusha, Ojung'u Salekwa, aliwashukuru wadau wa CCBRT kwa msaada huo muhimu kwa watoto wenye ulemavu.

Alisema licha ya watoto hao kuwa na changamoto lakini wazazi wao wanapitia matatizo mengi hasa katika malezi.

Pia, alisema kuna umuhimu kwa jamii kuungana na kutoa msaada wa hali na mali pamoja na kuwatia moyo familia zenye watoto hao.

Aidha, aliipongeza serikali kwa kuweka mazingira bora kwa wadau wa maendeleo kwa kuwa inathamini kazi kubwa inayofanya na wadau na aliwataka kuendelea kuisaidia serikali katika kuhudumia jamii hasa watoto wenye mahitaji maalumu.

Mratibu wa Huduma za viti mwendo kutoka CCBRT, Neophita Lukiringa, alisema lengo la kutoa msaada huo ni kwasaidia watoto kwenda shule na kufanikisha ndoto zao za elimu, pia kuwasaidia wazazi kurahisisha kazi ya kuwahudumia watoto hao.

Wazazi na watoto waliopewa msaada huo walishukuru kwa msaada huo na kusema ni huduma kwa kuwa watu wenye ulemavu wengi wanahitaji kwa ajili ya kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Fatuma Yusuph, mama wa Sahil Yusuph alishukuru msaada huo, huku akiiomba jamii kuendelea kuwasaidia wazazi wenye watoto wenye mahitaji maalumu kwa kuwa malezi ya watoto yana gharama na yanahitaji mzazi kutumia muda mwingi bila kufanya shughuli nyingine za uzalishaji.

Naye Rachel Mollel, mtoto aliyepewa kiti, aliishukuru serikali kwa msaada huo akisema kitamsadia kutembea akiwa shuleni na nyumbani pia.

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Arusha, Selema Msumi, alishukuru kwa msaada huo akisema kuwa halmashauri ina watoto 509 wenye uhitaji wanaosoma kwenye shule zenye vitengo maalumu, huku watoto 77 wakisoma kwenye Shule ya Bweni ya Ilboru.



Mtaalamu wa kutengeneza mashine kutoka Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (TEMDO), Mosses Chalamila (wa pili kushoto), akitoa maelezo kuhusu mashine ya kukamua mafuta ya mawese iliyobuniwa na taasisi hiyo kwa baadhi ya wakulima waliotembelea maonyesho ya wakulima Nanenane, Kanda ya Kaskazini katika viwanja vya Themi Njiro jijini Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Wakulima waitwa kukata bima ya kilimo mtetezi

**Na Mwandishi Wetu**

WAKULIMA wametakiwa kuyatumia maonyesho ya kilimo ya Nanenane kupata elimu ya aina mpya ya bima ya kilimo ya mtetezi.

Wito huo umetolewa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Bima ya Strategis-bima za majanga na mali, Jabir Kigoda wakati wa kilele cha maadhimisho hayo.

Alisema ni wakati muafaka kwa wakulima kupata elimu zaidi kuhusiana na bima hiyo jambo ambalo alisema litawaongezea maarifa kwenye shughuli zao za kilimo

Alisema watatoa elimu hiyo katika maeneo mbalimbali nchini ambako wakulima wanajumuika.

Alisema kuwa ujio wa bima ya mtetezi kunatimiza ndoto ya wakulima wengi na kwamba imekuja wakati muafaka ambapo wanaadhimisha mafanikio yao na kuangalia jnsi ya kuboresha mafanikio hayo.

Alisema mchango wa mtetezi katika malipo ya jumla kwa mwaka 2021 ulikuwa ni asilimia moja ambayo ni muda muafaka sasa kwa wadau wote wakuu kukusanyika ili kukuza bima hii.

Alisema kuwa faida za bima ya mtetezi ni pamoja na ulinzi wa fedha, usimamizi wa vihatarishi aina mbalimbali kwenye sekta ya kilimo, uboreshaji wa upatikanaji wa mikopo, uendelevu wa biashara, kuhimiza uwekezaji katika kilimo na kuhakikisha utulivu wa mawazo kwa wakuulima.

Alisema bima ya kilimo ya mtetezi hugharamia mazao mbalimbali, ikiwa ni pamoja na mazao makuu kama vile nafaka, mbegu za mafuta, kunde, mazao yenye asili ya mizizi, zao la miwa kwa ajili ya uzalishaji wa sukari na mazao aina mbalimbali ya kibiashara.

# Makinda: Tanzania inafanya vizuri utoaji taarifa za sensa

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

KAMISAA wa Sensa ya Watu na Makazi nchini, Anne Makinda, amesema Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazofanya uchambuzi mzuri na kutoa matokeo bora kwa kutoa taarifa za sensa ukilinganisha na nchi nyingine.

Aliyasema hayo juzi mkoani Arusha alipotembelea wataalamu wa takwimu nchini waliokuwa wameweka kambi mkoani humo kwa ajili ya hatua nyingine ya uchambuzi wa taarifa ya sensa inayoangazia kutoa takwimu za vizazi, uhamaji, walemavu na uhariri wa uchumi.

wametuma tena wataalamu kuja kujifunza zaidi namna ya kuendesha shughuli hii kwenye nchi yao," alisema Makinda.

Hata hivyo, aliwataka wananchi kuendelea kuwaamini wataalamu hao kwa kuwa wanaendelea na uchambuzi na alisema kazi ya kuandaa ripoti bado inaendelea kwa hatua inayaoendelea ni kuangalia taarifa za vifo, uzazi, uhamaji na uhariri wa kidemografia, kiuchumi na kijamii.

Alisema, kuna nchi nyingine huwa zinaishia kufanya sensa tu, lakini kutoa matokeo hazitoi kutokana na hatua nzima za utoaji matokeo zinavyohitaji muda mrefu kuchakata.

Naye Mratibu wa Sensa Taifa, kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu, Seif Kuchengo, alisema wamepata mtaalamu kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia idadi ya watu duniani, pia alieleza kuwa matumizi ya vishikwambi imewarahisishia kazi ya sensa na hadi sasa wamefikia asilimia 40 katika hatua ya pili.

Mwakilishi wa Mtakwimu Mkuu wa Serikali, ambaye ni Mkurugenzi wa Sensa ya Watu na Takwimu za Jamii, Ruth Minja, alisema wamekaribia kukamilisha ripoti ya taarifa ya sensa ya uchambuzi wa taarifa za vifo, uhamaji na hali ya ulemavu.

# Viongozi ushirika wawashtaki maofisa watendaji wa vijiji

**Na Jaliwason Jason,** BABATI

VIONGOZI wa vyama vya ushirika mkoani Manyara, wameiomba serikali kuwasaidia kuwadhibiti maofisa watendaji wa vijiji ambao wanawafukuza kwenye maghala ya vijiji vinavyotumiwa na Vyama vya Ushirika wa Kilimo na Masoko (AMCOS).

Walitoa ombi hilo jana wakati wakizungumza na katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara, Karolina Mthapula aliyemwakilisha mkuu wa mkoa huo, Queen Sendiga.

Mwenyekiti wa Maletadu AMCOS, Melick Sadeck Sulle, alisema Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Maletadu, amekuwa tatizo na anawakwamisha kutekeleza shughuli zao.

Sulle alisema mtendaji huyo ameshawapa ilani ya kuondoka kwenye ghala la kijiji hicho ambalo wanalitumia kufanya kazi zao.


Naye Michael Txasara, alisema chanzo cha watendaji wengi kuwanyang'anya maghala vyama vya ushirika lengo lao ni kuwakodisha maghala watu wengine ambao ni walanguzi.

Hata hivyo, alisema ushirika unahitaji mkono wa serikali ili uweze kuwasaidia wanaushirika na wakulima kwa ujumla.

Akijibu hoja za viongozi hao, Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara, Karolina Mthapula, aliahidi kulifanyia kazi malalamiko hayo juu ya watendaji wa vijiji ambao wanawasumbua.

Mthapula alisema, kuwa ni vizuri wawe wabunifu ili waweze kuongeza uzalishaji wenye tija kwa kuwa wanategemewa kukuza uchumi wa nchi.

Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoani Manyara, Absalom Cheliga, alisema AMCOS nyingi ziko hoi kiuchumi hivyo wataanzisha mfumo wa stakabadhi ghalani kwa ajili kuwakomboa wakulima katika mazao ya dengu, vitunguu swaumu na mbaazi.





# DC awataka mawakala wa fedha kujiimarisha kiulinzi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Johari Samizi, amewataka mawakala wanaotoa huduma za kifedha mkoani Shinyanga, kujiimarisha kiulinzi ili wasivamiwe, kuporwa fedha na kuuawa na majambazi.

Alibainisha hayo juzi wakati akizindua umoja wa mawakala wa huduma za kifedha mkoani humo na kusema kuwa shughuli ambazo wanazifanya mawakala hao ni kushika fedha, hivyo ni vyema wakajiimarisha kiulinzi ikiwamo kuajiri walinzi kwenye maeneo yao ya kutolea huduma za kifedha ili wawe salama muda wote.

"Natoa pole kwa kuondokewa na wakala mwezenu Richard Nzumbi ambaye aliuawa na majambazi walipomvamia kwa ajili ya kumpora pesa zake, nawasihi mjiimarishe kiulinzi kwa sababu shughuli zenu mnazofanya ni kushika pesa ili muwe salama," alisema.

Aidha, aliwapongeza kwa kuanzisha umoja wao akisema watafanikiwa kimaisha, kuwashauri pia kupitia michango yao wawaanze kukopeshana ili wakuze mitaji yao na kufikisha huduma hiyo ya kifedha maeneo mengi hasa vijijini.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na mawakala hao sababu wanatambua mchangao wao na hata makusanyo ya pesa za serikali za mapato maeneo ya vijijini hukusanywa kupitia mawakala kutokana huduma za kibenki kuwa mbali.

Naye Katibu Msaidizi wa umoja huo, Kwilasa Mahigu, alisema walianzisha umoja wao Februari mwaka huu baada ya kutokea tukio la mwenzao (Richard Nzumbi) kuuawa na majambazi, ndipo wakaona ni vyema wakawa na umoja wa mawakala kwa ajili ya kuwa na sauti ya pamoja.

Alisema pia umoja huo utakuwa ni kiungo muhimu cha kupeana taarifa juu ya fursa mbalimbali pamoja na kuanzisha Saccos ambayo watakuwa wakikopeshana fedha na kukuza mitaji pamoja na kusaidiana kwenye shida na raha.

# TIC yawaita wafanyabiashara kuwekeza kwenye kilimo

**Ndalike Sonda,** BARIADI

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC) Kanda ya Ziwa, kimewashauri wawekezaji hususani wafanyabiashara pamoja na wananchi wa mikoa hiyo kukimbilia fursa za uwekezaji katika kilimo.

Wito huo umetolewa juzi mkoani Simiyu na Meneja wa TIC, Pendo Gondwe, wakati akizungumza na Nipashe juu ya fursa za uwekezaji katika sekta mbalimbali.

Alisema kuwa sekta ya kilimo ni moja ya sekta za kimkakati nchini, hivyo ni vyema wananchi na wawekezaji kuipa kipaumbele na kuchukua hatua za haraka kuwekeza katika sekta hiyo.

Alisema kuwa katika kipindi cha miezi sita iliyopita TIC imesajili miradi 19 ya kilimo katika Kanda ya Ziwa ambayo inakwenda kutoa ajira 6,044 na mtaji wake ukitarajiwa kuwa wenye thamani ya zaidi ya Sh.bilion 334.9.

Gondwe alieleza kuwa zaidi ya miradi 1,200 ya usindikaji wa matunda imesajiliwa Kanda ya Ziwa na kati ya hizo miradi 74 ni miradi ya kilimo ambayo imeleta tija kwa wawekezaji wa Kanda ya Ziwa.

Alisema kuwa lengo la kituo hicho ni kutoa elimu kuhusu uwekezaji na kwa Kanda ya Ziwa wanahamasisha katika uwekezaji wa kilimo jambo ambalo wamelifanikisha kutokana na elimu ambayo imechangia kuongezeka kwa miradi hiyo.

Aidha, alieleza kuwa kituo hicho kinatarajia kuzindua mfumo wa usajili wa miradi kwa njia ya kieletroniki ambao utawarahisishia wawekezaji kusajili miradi na kufikia malengo katika kuinua kipato cha wakulima pamoja na taifa kwa ujumla.

TIC kilianzishwa mwaka 1997 chini ya Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 1997 na kwamba marekebisho ya sheria yaliyofanyika Novemba 2022, imeipa mamlaka kituo hicho kuhamasisha uwekezaji katika maeneo na sekta mbalimbali.



Askofu Mkuu wa kanisa la Anglikana Tanzania, Dk. Mahimbo Mndolwa (kushoto), akiwaelekeza wachungaji wakati wakiingiza jeneza lenye mwili wa aliyekuwa Mshauri wa wanafunzi Chuo Kikuu cha St. John cha Dodoma, Mch. Patrick Bendera katika kanisa la Anglikana la mtaa wa Madaba, mjini Muheza mkoani Tanga juzi, kwa ajili ya ibada na baadaye maziko yake wilayani humo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Serikali yashauriwa kufufua viwanda vya pamba

**Na Shaban Njia,** KAHAMA.

MADIWANI wa Halmashauri ya Ushetu mkoani shinyanga, wameishauri serikali kupitia Wizara ya Kilimo kufufua viwanda vilivyokuwa vinanunua na kuchakata pamba ili kuongeza uzalishaji wa zao.

Inaelezwa kuwa kwa sasa kipo kiwanda kimoja tu cha Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), kinachonunua na kuchakata zao hilo hali ambayo inaleta ushindani wa bei na viwanda vingine vya kuchakata zao hilo na kusababisha wakulima kuongeza uzalishaji na kupata fedha za kujikimu kimaisha.

Akizungumza katika kikao kazi cha kuweka mikakati ya uendelevu wa kilimo cha mazao ya chakula na biashara kupitia mradi wa PETS, Diwani wa Kinamapula Halmashauri ya Ushetu, Sharifu Samweli ,alisema kuwa ili kilimo cha zao la pamba kikue kama yalivyo mazao mengine serikali inapaswa iweke mkono wake.

Alieleza kuwa kupitia Wizara ya Kilimo wanatakiwa kuhakikisha inaelekeza nguvu katika kufufua viwanda vilivyokufa vya kuchakata zao hilo vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika hali itakayoongeza uzalishaji na ushindani wa bei kila mwaka.

Samweli alisema msimu wa kilimo uliopita bei ya pamba kwa kilo moja ilikuwa Sh. 1,600 lakini kutokana na KACU kununua pia ushindani wa bei ulikuwa mkubwa na kusababisha wakulima kuuza kwa Sh.2,200.

"Msimu huu walikuwa wengi wameacha kulima mahidi na mpunga na kukimbilia kulima zao hili kutokana na bei yake kuwa nzuri, lakini imeshuka bei hadi Sh.1,060 hali ambayo inakatisha tamaa ya kuendelea kuzalisha zao hili. Ili likuwe kama mazao mengine serikali ifufue viwanda vilivyokufaa," alisema Samweli.

Diwani wa Igunda, Tabu Kato ,alisema wakulima wanaacha kulima zao hilo kutokana na bei zake kutoelewa kila mwaka kulinganisha na bei ya tumbaku ambayo inapangwa kabla ya kulima.


Alisema wakulima wanalazimika kuuza kwa bei hiyo kwasababu hawana uwezo wa kukaa nayo ndani kusubiria bei ipande.

Awali mwezeshaji wa mradi wa Pets, Dickson Maganga alisema, moja ya sababu inayosababisha kilimo kushindwa kukua ni wakulima kutozingatia ushauri wa kitaalamu kwa kisingizio kuwa wakilima kwa kufuata utaalamu unawaongezea gharama shambani.

Mwenyekiti wa Chama cha Wasioona Mkoa wa Shinyanga, Marco Nkanjiwa alisema, kupitia mradi wa Pets wanaotekeleza katika kata sita za mkoa huo watahakikisha wanawafikia wakulima wengi zaidi ili kuhakikisha mazao ya chakula na biashara uzalishaji wake unaongezeka.


Ukurasa 12

Umasikini, elimu duni na ndoa za utotoni inavyozalisha utapiamlo unaotisha Njombe



Ukurasa 13

Hivi marufuku zetu zina meno au kibogoyo?


Ukurasa 14

**Zijue ajira za muda zinazoendeshwa na TASAF katika ukanda wa Pwani**

BUFE
IJUMAA AGOSTI 11, 2023
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

UCHUMI

# Wanahabari wasukwa safari kusaka maendeleo kupitia jinsia na dijitali

**Na Yasmine Protace, aliyekuwa Morogoro**

HADI sasa kasi ya maendeleo duniani inashuhudiwa kuwa juu zaidi. Moja ya wakala mkuu katika hatua hiyo, ni ubora katika mfumo wa mawasiliano, hapo nyenzo kuu ikiwa teknolojia ya dijitali.

Jirani na fani hiyo, nafasi inashikiliwa na mdau mwandamizi wa mahali hapo, kundi la wanaopita wanahabari, wakivitumikia vyombo ambavyo vimo katika mifumo ya mikuu ya maandiko - magazeti, elektroniki kwa njia ya redio, televisheni na mifumo ya kidijitali.

Kimkakati, dhana hiyo ya maendeleo pia inamuangalia aliye muhimu katika uhusiano wa jinsia, wanawake kitakwimu nchini na duniani, ndio wako wengi zaidi.

Hivyo, ili kumkwamua kiuchumi mwanamke, kwanza inatajwa kuwa ya lazima, ikiwasaidia wanawake wengi kujikwamua kiuchumi, vilevile kujiongezea vipato. Ndani ya mtazamo huo, ni hivi karibuni Muungano wa Klabu za Waandishi wa Habari (UTPC), uliandaa mafunzo maalum yalilyolenga usawa wa kijinsia na mustakabali wa kiuchumi kwa wanahabari.



Mshiriki Mkufunzi, Hilda Kileo, akiwapa somo wanahabari, mwelekeo mpya wa kuyaona maendeleo, kupitia mtaji wa jinsia na teknolojia ya mawasiliano. **PICHA: MTANDAO**

Hilda Kileo, ni Ofisa Programu kutoka UTPC, ambaye pia ni Ofisa Miradi, ambaye pia anashughulikia usawa wa kijinsia, anaitaja elimu ya kidijitali kwa sasa ndio mkombozi wa mwanamke.

Katika mada yake kwenye mafunzo yaliyofanyika mjini Morogoro, katika mada aliyoitoa kwa waandishi wanafunzi kutoka klabu mbalimbali za habari nchini, anasisitiza elimu ya dijitali kwa wanawake, ili watumie zana na teknolojia hiyo.

Anaorodhesha yanayoendana na dijitaIi, yanajumuisha vitendea kazi kama intaneti, kushiriki kimtandao au 'zoom meeting' na kutathmini taarifa za mtandaoni.

Kuhusu uwezeshaji, kinamama na ujasiriamali, Hilda anasema teknolojia ya mawasiliano inabaki kuwa chombo chenye nguvu kinachowawezesha wanawake kwa kuwapa fursa ya kupata taarifa na kushiriki biashara za mtandaoni, ikiwamo kimataifa.

"Majukwaa ya mtandaoni yanaweza kuwawezesha wanawake kuanzisha biashara na kukua kwa biashara," anasema Hilda.

Pia, anafafanua kwamba ni teknolojia inayoongeza fursa za elimu kwa wanawake, hasa katika maeneo kunakokosekana fursa za kutoka na kwenda kupata elimu darasani.

Anasema kozi zinazotolewa mitandaoni, zinamuwezesha mama kujifunza na kukuza ujuzi, hata akavunja vizuizi vya kijiografia vinavyomkabili, kwa kuboresha ufikiaji wa wanawake kwenye taarifa na huduma za afya kwa programu za simu za mkononi zinazohusiana na afya ya mama kupanga uzazi na ustawi wa ujumla.

Akizungumzia wanawake na teknolojia, anasema usawa wa kijinsia na uwakilishi, ni kuongeza uwakilishi wa wake katika teknolojia hiyo muhimu, ikikuza usawa wa wanawake katika sekta.

Hilda anafafanua kuhusu juhudi za serikali, akisema kuna nchi nyingi zinafanya kazi ya kutekeleza sera hizo kuziba pengo la kijinsia katika eneo la teknolojia ya mawasiliano ya habari.

"Juhudi hizo zinawezesha kujumuisha mafunzo ya ujuzi kwa digitali kwa wanawake, kwa kuunda programu za kuwaongoza na kuendeleza sera zinazojali jinsia katika teknolojia," anasema.

Eneo lingine shirikishi analitaja suala la maendeleo endelevu ya usawa wa kijinsia, kwa kuzingatia kuingizwa wanawake katika Teknolojia ya Mawasiliano ya Habari na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa, hususan inayohusika na Usawa Kijinsia na Viwanda, Ubunifu na Miundombinu.

Mkufunzi, Deo Temba, anasema lengo kuu la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo waandishi kuandika habari zenye usawa wa kijinsia na mambo ya kuzingatia wakati wa kuchambua habari kwa mtazamo wa kijinsia.

Anakumbusha haja ya kuandikwa habari kwa uwiano sawa ndani ya jinsia tofauti zilizopo.

Mkurugenzi Mtendaji wa UTPC, Kenneth Simbaya anasisitiza, ili kuwapo maendeleo endelevu, kuna haja ya kuzingatia hatima ya jinsia katika jamii husika, akiwahimiza waandishi wa habari wasirudi nyuma katika kuandika habari za kijinsia.

UCHUMI

# Umasikini, elimu duni na ndoa za utotoni inavyozalisha utapiamlo unaotisha Njombe

**Na Elizabeth John,** Njombe

MKURUGENZI wa shirika la Safina Association, Eunice Lwendo, anasema kuwapo kwa janga la ndoa za utotoni mkoani Njombe, kumechangia tatizo la utapiamlo unaosababisha udumavu kwao.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Awali ya Viashiria vya Uzazi na Mtoto na Malaria Mwaka 2022, katika Kanda ya Nyanda za Juu Mkoa wa Iringa inakadiliwa kwa wastani wa asilimia 56.9, Jirani yake Njombe asilimia 50.4 ikifuatiwa na Rukwa asilimia 49.8.

"Hawana elimu ya malezi, wanalazimishwa kuingia kwenye ndoa bila ya maelekezo yoyote yale, anakua hajapata mafunzo yale ambayo yanaweza kumtosheleza ili kuingia kwenye malezi," anasema na kuongeza.

"Madhara makubwa yanakuja kwenye malezi ya watoto. Mtoto huyu anayemzaa mtoto mwingine hawezi kujua namna ya kumlea mtoto, ndipo tunakuja na udumavu, suala la udumavu Njombe linatokana na si kwamba Njombe hakuna vyakula Hapana.

"Bali jinsi wale wazazi wake na mama mwenye watoto kujua namna ya kuwatayarishia watoto na wao wenyewe kula chakula kizuri ambacho ni 'balanced diet' (mlo kamili).

"Hawa watoto wadogo wanaoenda kupata Watoto, wanakuwa hawajui kabisa namna ya kuweza kujitunza wenyewe na kutunza watoto wao," anasema.

Ni kauli ya Mkurugenzi Lwendo, akifafanua Mradi wa Asasi ya Child and Women Empowerment, unataja kuwa wasichana hao wadogo wanaingia kwenye ndoa bila ya kuwa na maarifa au ujuzi wa elimu ya lishe bora.

"Sisi tulibaini hicho wakati tunakwenda kwenye hizo kliniki. Mara nyingine tulikuwa tukifuatilia, tulikuwa na programu moja tulikuwa tunashughulika na watoto wadogo na wazazi wenye watoto wadogo, ndipo tulipogundua kwamba watoto wengi walio kwenda kwenye kliniki hawana ujuzi wowote kuhusu uzazi.

"Wao wenyewe kwanza hata kusema kama ni mjamzito ana mimba kwao ilikuwa ni kitu cha kushangaza," anaeleza Lwendo. Mwenye ufafanuzi wa ziada:

"Tatizo la ndoa za utotoni ni kubwa sana, kwa sababu wengi wakimaliza hata shule ya msingi, wale ambao hawafanikiwi kwenda sekondari, unakuta wanajiingiza kwenye masuala ya biashara ndogondogo, lakini wakishindwa unakuta tayari wanaolewa wakiwa bado ni wadogo."

Ana la ziada: "Hata ukipita sokoni au barabarani utakutana nao wamejitwisha madishi wanatembeza matunda na mbogamboga, lakini ukiwaangalia ni watoto bado hawajawa watu wakubwa kusema kwamba wanahimili familia zao."

Kwa mujibu wa Lwendo, wasichana wengi hujiingiza kwenye ndoa za utotoni, kutokana na umasikini ambao unasababisha kuanzisha familia wakiwa bado wadogo.

"Jingine ni masuala ya elimu, akiona amemaliza la saba au kidato cha nne hana mwelekeo, unakuta anaamua kwamba kinachofuatia ni kuolewa tu!" anasisitiza Lwendo.

Mkurugenzi huyo anataja changamoto nyingine kwenye suala juu ya ndoa za utotoni, ni Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, inayomruhusu msichana mwenye umri wa miaka 14 kuolewa.

Katika hilo analalamika kwamba: "Hapa hapako sawa, kwa sababu wanakuwa hawajakomaa hata viungo, wanapopata mimba wanapata shida. Kwa hiyo, sheria ingeangalia upya kipengele hiki."

Pia, anafafanua kwa mapana madhara mengine ya ndoa za utotoni, ipo katika akili ya binti anakuwa bado hajapevuka katika nafasi ya kutunza familia, hali inayoweza kuwa chanzo cha migogoro na yule anayemuoa.

Ananena kwamba muoaji anajihsi ana mwenza aliyekomaa kiakili, lakini katika uhalisia ni mtoto ambaye kimsingi, hawezi kubeba majukumu ya mama kwenye familia.

Maoni yake ni kwamba kukifanyika marekebisho katika Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, yatasaidia haraka kuondoa upenyo wa kuhalalisha ndoa za utotoni, kwani zimekuwa na madhara makubwa kijamii.

Lingine analohimza, ni haja ya kuwapo elimu zaidi kwa watoto wanaomaliza shule, jinsi ya kuendelea kujitegemea kabla ya kufahamu daraja la mapema, akisisitiza: "waelezwe athari za uzazi au kuolewa mapema."



Wakazi mji wa Njombe wakiwa kwenye mkusanyiko, wakipatiwa elimu ya lishe. **PICHA ZOTE: MAKTABA**



Mkurugenzi wa Shirika la Safina Association, Eunice Lwendo la mjini Njombe. **PICHA: ELIZABETH JOHN**

> "Jingine ni masuala ya elimu, akiona amemaliza la saba au kidato cha nne hana mwelekeo, unakuta anaamua kwamba kinachofuatia ni kuolewa tu!

### WANAVYOELEZA WAKAZI

Vumilia Mgina, mkazi wa Njombe, anasem wanaotumbukia katika ndoa za utotoni, wengi hawana elimu sahihi ya lishe, mzizi mkuu ukiwa katika athari ya kutoandaliwa kwa majukumu hayo, pia kutokana na upeo wa akili zao kuwa mchanga.

"Nilimaliza shule sikupata nafasi ya kuendelea na masomo ya sekondari nilikaa mtaani mwaka mmoja maisha yakawa magumu nikaolewa, lakini changamoto ilikuja nilivyopata mtoto, maana kila nikimpeleka kliniki alikuwa haongezeki uzito.

"Siyo kwamba alikuwa anaumwa, ila tu uzito ulikuwa hauongezeki nikaambiwa ana utapiamlo," anasimulia Mgina ambaye, kama walivyo mabinti wengine, naye alijikuta ametumbukia kwenye majukumu ya ndoa angali mdogo wakati huo akiwa na umri wa miaka 16.

Anasimulia mkasa wake kwamba, alisukumwa kuingia kwenye maisha ya ndoa mapema, kwa sababu ya shinikizo la changamoto za maisha zilizomkabili.

Joseph Sanga mkazi wa Njombe Mjini, anaiasa jamii kuacha tabia ya kuwaozesha watoto kwenye umri mdogo, kwa sababu wanawatwishwa majukumu ambayo kwa umri wao hawayahimili.

### OFISA LISHE

Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, mkoa wa Njombe, Samson Mwitambe, anakiri kwamba msichana anapoingia kwenye ndoa za utotoni, tayari anakuwa hana elimu sahihi inayohusu lishe na afya kwa ajili ya mtoto.

"Ni kweli kwamba kuna mahusiano makubwa sana kati ya lishe ambayo ni viini lishe na vinasaba vya wanadamu. Sasa tunapozungumzia udumavu, ina maana hajawa mrefu kulingana na umri alionao na urefu alionao sasa mtoto.

"Kama mama hajapata maumbile ya kuandaa mwili wake ili kupata mimba, ina maana mtoto ambaye atakuwa ametungishwa aidha kwa bahati mbaya, kubakwa au yeye mwenyewe kataka inawezekana akapata udumavu.

"NI kwa sababu 'viyai' vya uzazi ambavyo vitasababisha mtoto yule aweze kufyonza vyakula kupitia 'plasenta' (mfuko wa uzazi) vile 'viyai' vya uzazi vinakuwa havijawa na lishe za kutosha. Inaweza ikamfanya yule mtoto akapata udumavu," anasema Mwitambe.

"Vile vile huyu mtoto inawezekana kabisa mama ana virutubisho kwenye mwili wake akajifungua yule mtoto, lakini malezi baada ya kuwa amejifungua yakawa kidogo kipato hana.

"Kwa hiyo, ina amana kuwa mtoto huyu anashindwa kupata chakula stahiki. Anaweza kudumaa kwa sababu vyakula anavyopata sio sahihi," anafafanua.

Mwitambe anaeleza hoja ya watangulizi kuwa wasichana wanapoolewa katika umri mdogo, wanakuwa hawajajiandaa kwa malezi bora na sahihi.

"Inawezekana kuna chakula kinapatikana, lakini ile hali ya kumlisha inatakiwa kumuangalia mtoto ale, lakini anakuwa siyo muangalifu. Inaweza ikasababisha yule mtoto akapata maradhi yatokanayo na vyakula.

"Inamfanya anaumwa muda mwingi, kukua kule kunakuwa hakupo tena, vilevile vyakula vinavyosababisha mtu kukua havipati na kama anavipata ni kidogo sana, havikidhi mwili wake," anaeleza Mwitambe.

### DAKTARI BINGWA

Mtaaluma bingwa wa tiba ya kinamama katika Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Njombe, Dk. Shomari Masenga, anasema suala la lishe duni katika ndoa za utotoni, linabeba madhara kwa binti aliyebeba ujauzito.

Hapo anafafanua kwamba inamsababishia viungo vyake vinakuwa bado havijakomaa kukidhi kazi hiyo na hata kuhatarisha hatua yake ya kujifungua.

Dk Masenga anasema, madhara mengine kwa binti huyo yanaweza kuwa ni kupata shinikizo la uzazi, likamsababisha kifafa cha mimba au kujifungua kwa upasuaji, kwa sababu nyonga zinakua hazijakomaa.

"Maana yake nyonga zao ni ndogo, ndiyo maana wakati mwingine wanaishia kufanyiwa upasuaji, lakini kama atachelewa kwenda kufanyiwa, maana yake atapata uzazi pingamizi na uwezekano wa kupata fistula pia upo," anasema Dk. Msenga.

Tabibu huyo anasema, umri mdogo na kutopevuka kiakili kunampotezea mama uwezo wa kumlea mtoto, kwa sababu ya hali ya kiuchumi na anashindwa kumpa mtoto haki za kijamii ikiwamo elimu na afya.


"Huyu mzazi ambaye na yeye ni mtoto anaweza akashindwa kumlea mtoto, kwa sababu yeye huenda hayupo vizuri kiuchumi, kwa hiyo atashindwa kumpa haki zake kama elimu na afya," anasema Dk. Masenga.



Hali ya uzazi katika umri mdogo.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Hivi marufuku zetu zina meno au kibogoyo?






**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**kulangwasos@gmail.com**

SIKU za awali kabisa za utawala wa Rais, Dk John Pombe Joseph Magufuli ziligubikwa na marufuku kadhaa hivi, zikilenga kuweka watu sawa badala ya kufanya mengine ila wajikite katika kazi.

Ndipo siku alipoibuka na kaulimbiu yake maarufu ya 'Hapa Kazi Tu', kila mtu akaimba kivyake na kauli hiyo ikashika kasi na watu kwa kweli wakafanya kazi, hata ofisini ambako kulikuwa na kuringaringa, watu wakanyooka.

Katika marufuku hizo, ikawamo ile iliyogusa wenye nazo ya ukitaka kusafiri nje ya nchi, mpaka kwa ruhusa ya Ikulu, kutoka kwa mkubwa mwenyewe, yaani alisema mnatumbua na kutumia vibaya fedha za umma.

Alinifurahisha pale aliposema huko ughaibuni kuna mabalozi, kwanini tunawateua, kwani huko wanakwenda kustarehe tu mpaka sisi tutoke huku kwenda kufanya kazi ambazo wangeweza kuzifanya?

Akasema kama ni wazungu wanatuhitaji, watatufuata hapa hapa Bongo. Watu acha wakasirike, acha wanune. Wakaanza kuhoji, sasa maendeleo yatatoka wapi bila sisi kwenda huko?

Sisi kina pangu pakavu tia mchuzi, tukawa tunachekelea nyoyoni tu, huku tukiwananga waliokuwa wanahifadhi mabegi uwanja wa ndege na kubadilishia suti hapo, kwamba sasa kiko wapi, tutakuwa tunatazamana nao hapa hapa. Yaani tubanane hapahapa kwenye ardhi ya JPM.

Walinuna mpaka wakazoea, chini ya marufuku ya John. Wakawa wanamtazama mtangulizi wake kwa jicho kali, kwamba ndiye aliyemleta mtu wake huyo madarakani na hasa aliposhindilia akisema "nakuleteeni chuma hicho na kimeanza kutoa checheeee."

Waliozoea kubadilisha ndege wakatamani wahame nchi, kwa sababu sasa utakwenda Ikulu kumwambia nini JPM, eti unataka kwenda nje, kutafuta nini? Unajua kabisa nje wapo mabalozi kiranga cha nini?

Wakati tukishangilia sisi walalahoi, mara akaja na marufuku nyingine, kwamba kuanzia sasa marufuku baa kufunguliwa asubuhi badala ya kufanya kazi, akasema sana sana baa imewahi kufunguliwa, ni saa 10 jioni na saa sita usiku, mwisho.

Mtu wa kwanza aliyesikia hilo na kuja kunilalamikia ni rafiki yangu mlinzi wa usiku wa baa fulani pale Chang'ombe, ambaye hakusita kunitamkia akiwa nazo kichwani, kuwa huyu Rais sasa hatufai, kwa sababu muda huu anataka tufanye nini?

Nikajikuta namjibu kuwa anataka tufanye kazi, akanitazama usoni kama vile si rafiki yangu wa siku nyingi, akajibu sasa mimi kwa mfano, nimetoka kazini asubuhi, nifanye kazi gani tena kama si kukaa nyumbani nigombane na familia?

Akasisitiza kuwa hizi marufuku wakati mwingine hazina maana zaidi ya kutafutana ubaya. Nikamwuliza sasa anataka afanye nini? Jibu rahisi kabisa ni kwamba namwachia Mungu, kwa sababu hii haitadumu na si ya muda mrefu itafika mwisho.

Sikumjibu kitu, ila nikajisemea tu rohoni kuwa kumbe jamaa hamjui huyu 'meti' wangu, kwamba ni mtata ile mbaya, nikamkumbusha jinsi alivyoambiwa kuchukua fomu ya urais kabla hata hajafikiria, akajibu kuwa "watalimia meno!"

Nikataka kumwambia kuwa sasa ajiandae kulimia meno, nikaona nitampandisha hasira asije akaning'oa haya ya kwangu kabla nami sijaanza kuyalimia. Nikamtia moyo tu kuwa yana mwisho.

Nilimwambia yana mwisho kwa kumkumbusha marufuku nyingi zinazotolewa nchini na zisifuatwe, kwamba ni kama maneno ya msimu tu huja yakaisha. Mnakumbuka semi kama "ndege itatua au haitui?" Mnakumbuka vijana wa siku hizo mlipokuwa mnatongoza? Ni misimu ilishapita hiyo.

Hamkumbuki tulishapigwa marufuku ya kuuza mapanga na visu mitaani? Mnakumbuka tulishatwishwa marufuku ya daladala kutoweka mafuta kituoni ikiwa na abiria? Mnakumbuka kuna marufuku ya kutotumia simu kwenye kituo cha mafuta?

Kwani mnadhani hakuna marufuku ya kutupa taka ovyo barabarani? Au ya dereva wa bodaboda kutovaa kofia ngumu na kutosimama kwenye mataa ya kuongoza vyombo vya moto barabarani?

Zipo marufuku za kulewa ukaendesha gari, marufuku za kucheza kamari, lakini zinafuatwa? Kamari siku hizi ni sehemu ya maisha, hasa kwa vijana tena masikini.

Ulishasikia kamari zinazoitwa bahati nasibu, akashinda mwalimu, polisi, mwanajeshi au kiongozi? Utasikia mimi ni mama lishe, fundi rangi, dereva bodaboda, fundi vyuma, muuza chipsi, kondakta na wale wa chini chini tu kiuchumi, kumbe tunapiga marufuku kamari, lakini huku tukizitumia kama vigezo vya kukuza wajasiriamali. Marufuku au geresha? Alamsiki!

UCHUMI

# Zijue ajira za muda zinazoendeshwa na TASAF katika ukanda wa Pwani

**Na Beatrice Moses**



Wahusika wa TASAF mkoani Pwani wakiwa katika shughuli zao. **PICHA: MTANDAO**

MIRADI ya kutoa Ajira ya Muda kwa Kaya masikini inayoratibiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), inatajwa kuwa mpango bora unaolenga kunusuru kaya hizo na kuzifanya zipige hatua katika njia ya kujitafutia kipato, sanjari na kutoa ujuzi wa kazi kwa wahusika.

Katika taarifa iliyotolewa na Mtaribu wa TASAF Mkoa wa Pwani, Roeline Kimaro, kuhusu miradi ya kutoa ajira za muda kwa walengwa kwa Mkoa wa Pwani, inatekelezwa katika halmashauri nne anazozitaja kuwa za Bagamoyo, Chalinze, Kibaha Kisarawe.

"Muda wa utekelezaji wa miradi hii kwa walengwa ni siku 60 kwa mwaka, ikiwa ni siku 10 kwa mwezi kwa muda wa miezi sita kwa kila halmashauri.

"Lengo la miradi hii, ni kutoa fursa kwa kaya zenye wanakaya wenye uwezo wa kufanya kazi kushiriki katika utekelezaji wa miradi na kulipwa ujira," anabainisha Kimaro

Anasema kufikia mwaka fedha 2021/2022 miradi ya muda iliyotekelezwa ni 168 na iliibuliwa katika vijiji 140 na kutekelezwa na walengwa 3,362 walionufaika na ujira wa jumla shilingi 476,784,00, pamoja na fedha za ununuzi wa vifaa shilingi 148,108,270.

Pia, inatajwa awamu ya pili imetekelezwa hadi Februari mwaka huu, ikiibuliwa miradi 130 katika vijiji 200 na inatekelezwa na jumla ya walengwa 5754. Anafafanua kuwa, hadi sasa fedha zilizotolewa kwa ujira ni kiasi cha shilingi 729,930,000 na vifaa shilingi 148,108,270.

**MPANGO WA AKIBA**

Inatajwa suala la kuweka akiba na kukuza uchumi wa kaya kumewajengea uwezo walengwa mkoani Pwani, hasa katika kutunza rasilimali, kutengeneza njia mbadala na endelevu za ajira na kushiriki katika kazi za jamii.

Halmashauri za mkoa wa Pwani, hutoa ruzuku za uzalishaji kwa walengwa, ambazo ni wilaya za Bagamoyo na Kibaha, zikiwa na masharti kadhaa:

Mosi, kaya husika ni lazima ipatiwe mafunzo ya stadi za msingi za shughuli za kiuchumi na ujasiriamali; iwe na nguvu kazi; iandae mpango rahisi wa biashara; iombe kupatiwa ruzuku ya uzalishaji; iwe imejiunga na vikundi vya kuweka akiba na kukuza uchumi wa kaya (vya TASAF), ambavyo kwa sasa vimepata usajili wa Benki Kuu ya Tanzania (BOT) na halmashauri zao.

Mkoa wa Pwani katika halmashauri zake zote tisa, inatajwa kufanikiwa kuunda vikundi vya walengwa 1,478 vya akiba, vyote vimesajiliwa kwenye mfumo wa huduma ndogo za kifedha wa BOT na mfumo wa TASAF (MIS).

"Jitihada hizi za kuunda vikundi hivi vya kiuchumi kwa walengwa wa mpango zimepelekea baadhi ya walengwa kukidhi masharti ya kunufaika na ruzuku za uzalishaji kutoka TASAF na vikundi vya TASAF, kupata mikopo inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri," anasema Kimaro.

Anatoa mfano wa Halmashauri ya Wilaya Rufiji, tayari wameshatoa shilingi 6,500,000 kwa kikundi cha Tujumuike, chenye mradi wa kilimo cha ufuta.

**MIRADI YA UJENZI**

Kimaro anasema, mkoa wa Pwani umeendelea kunufaika na utekelezaji miradi ya miundombinu, kwa mwaka 2021/2022, jumla ya miradi minne yenye thamani shilingi 459,242,281.42 ilitekelezwa katika halmashauri mbili: wilayani Rufiji miradi miwili, ya ujenzi wa soko la kisasa Utete na Shule ya Sekondari ya Wasichana Mama Samia.

Kibaha nako kunaorodeshwa miradi miwili, ujenzi wa zahanati ya Mwanalugali na nyumba ya watumishi Vikawe.

Lingine analotaja Kimaro, ni mwaka wa fedha uliopita, 2022/2023 mkoa ulipangiwa fedha za miradi 3 katika Halmashauri ya Wilaya Kibiti Ujenzi wa Majengo matano katika Kituo cha afya wenye thamani ya shilingi 46,006,356 wilaya ya Chalinze chumba cha kuhifadhia maiti (mortuary ccomplex) 11,956,9497.32.

Kuhusu utekelezaji wa kuvutia wa ujenzi wa soko la Utete, inatajwa mafanikio yake , hata kuwafanya watendaji kutoa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Kamati ya Usimamizi kutoka Shehia ya Kizimkazi kufanya ziara ya siku mbili ya Mei 30 na 31 mwaka huu (2023) kujifunza namna ya uendeshaji wa miradi kadhaa inayotekeleza wilayani Rufiji, Pwani.

**NENO LAO WATEKELEZAJI**

Awali, mtaalamu wa masuala ya uchumi Profesa Haji Semboja, akaiambia Nipashe, kwamba mpango kama huo umekuwa ukifanywa kwenye nchi nyinginezo na kutoa fursa kwa walengwa kujiingizia kipato kinachowasaidia kujikwamua kiuchumi,wakapiga hatua zaidi.

"Wale wanaoshiriki kwenye ajira hizo kama ni za ujenzi wa barabara, au uvunaji, wanapata uzoefu kwenye kazi hizo. Naona TASAF ina mwelekeo mzuri wa kuzikomboa kaya hizo kiuchumi," anasema Profesa Semboja .

Meneja wa Miradi ya Ajira za Muda na Uendelezaji wa Miundombinu wa TASAF, Paul Kijazi, anasema utaratibu wa kuwapa ajira hizo wanufaika wa mpango huo, unahusisha miradi inayoibuliwa na wanajamii wenyewe, kwa kuangalia changamoto zilizopo kwenye maeneo yao.

Anasema, miradi hiyo inaweza kuwapo kutokana na ukosefu wa daraja, kisha ikaunganishwa na wanakijiji, pia huduma mbalimbali za kijamii kama vile za afya na elimu, kwenye mahitaji kama ya kukosekana barabara, zahanati, matundu ya vyoo shuleni au vyumba vya madarasa.

> **Pia, wanaopaswa kufanya kazi ni walio na umri kati ya miaka 18 na 65. Watu wenye ulemavu, wajawazito na kinamama wenye watoto chini ya miaka miwili hawahusishwi.**

Pia, anafafanua namna nguvukazi hutolewa, inapotokea mwakilishi wa kaya ana udhuru, basi anajitokeza wa kumwakilisha ili nafasi ya nguvukazi hiyo isikosekane.

Meneja huyo wa TASAF, anafafanua kwamba walengwa watafanya kazi kwa siku 10 kila mwezi ambao ni wastani wa siku 60 au miezi miwili kwa mwaka.

Kila siku anasema atafanya kazi isiyozidi saa nne kwa siku, kutekeleza yale aliyopangiwa siku hiyo.

TASAF inabainisha kuwa ujira unalipwa kwa kazi kulingana na idadi ya siku za mshiriki alizofanya kazi, kwa wastani wa shilingi 3,000 kwa siku, ikiunda malipo ya shilingi 30,000 katika kila mwezi kutokana na siku 10 anazofanya kazi.

Kwa mujibu wa Kijazi, ni shughuli inayotekelezwa kwa kuzingatia jinsia, pia Mwongozo wa Usimamizi wa Mazingira na Kijamii.

Pia, wanaopaswa kufanya kazi ni walio na umri kati ya miaka 18 na 65. Watu wenye ulemavu, wajawazito na kinamama wenye watoto chini ya miaka miwili hawahusishwi.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kwembe, uliopo katika wilaya ya Ubungo, Dar es Salaam Barnabas Asenga, anasema katika eneo lake ana kaya 60 zilizopo kwenye mpango wa TASAF, lakini bado hajapokea taarifa kuhusu miradi hiyo ya ajira za muda, hivyo anajitayarisha kuisimamia kuhakikisha inafanikiwa kufikiwa malengo.





Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye ulemavu, Patrobas Katambi (wa tatu kulia), akikabidhi cheti cha ushindi wa pili wa Taasisi za serikali kwa Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joshua Ng'ondya katika kilele cha maonyesho ya wakulima Nanenane Kanda ya Kati katika viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma juzi. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# TEA kutumia bil.4/- kufadhili miradi ya elimu shule 81

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Elimu Tanzania (TEA) imepanga kutumia Sh.bilioni nane katika mwaka wa fedha 2023/24 kwa ajili ya kufadhili miradi ya kuboresha miundombinu ya elimu nchini kwenye shule 81. Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Bahati Geuzye, alisema miradi hiyo itakapokamilika itanufaisha wanafunzi 39,484 na walimu 169 wa shule za msingi na sekondari. "Fedha hizi zitatumika kufadhili miradi 82 katika shule 81 zikiwemo za msingi 48 na sekondari 33 zilizopo maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara," alisema.

Alibainisha miradi itakayofadhiliwa ni pamoja na ujenzi wa madarasa 82, matundu ya vyoo 336, mabweni 10, ujenzi wa maabara 18 za masomo ya sayansi na nyumba za walimu 32.

Kadhalika, alisema kwa mwaka huo, Mfuko wa Elimu wa Taifa utatoa ufadhili kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu na kuwezesha ununuzi wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika taasisi moja ya elimu ya juu Tanzania Zanzibar utakaogharimu Sh.milioni 300.

Alisema katika mwaka 2018/19 hadi mwaka 2022/23, Sh.bilioni 20.1 zimetumika katika utekelezaji wa miradi kwenye taasisi 235 chini ya mfuko wa kuendeleza ujuzi.

"Taasisi zilizopata ufadhili zimetekeleza programu za mafunzo ya ujuzi kwa vijana katika sekta za kilimo na kilimo uchumi, TEHAMA, utalii na huduma za ukarimu, nishati, ujenzi na uchukuzi," alisema. Alibainisha kuwa watu 49,063 wamenufaika sawa na asilimia 114 ya walengwa, kati yao wanawake 22,413 sawa na asilimia 46 na wanaume 26,650 sawa na asilimia 54 ya wanufaika wote.

# Hatua tisa kushirikisha vijana kukuza ujuzi wa ajira zatajwa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SERIKALI imetaja hatua tisa zilizochukuliwa za kuwashirikisha vijana kwa ajili ya mustakabili wa taifa ikiwamo kuwawezesha vijana kuwa na ujuzi unaohitajika katika soko la ajira.

Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof.Jamal Katundu aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Vijana Kimataifa ambayo hufanyika kila ifikapo Agosti 12.

Alisema kupitia programu ya kukuza ujuzi vijana wamepata fani mbalimbali kama vile TEHAMA, uashi, useremala, ushonaji, ufundi bomba, uchomeleaji na uungaji vyuma, ufundi magari, ufundi umeme, ukarabati wa bodi za magari, upishi na uhudumu katika hoteli.

"Kupitia programu hii vijana 121,898 wamefaidika tangu mwaka 2017 hadi Juni 2023 na kati ya wanufaika hao, vijana 91,106 wamepatiwa ujuzi kupitia mafunzo ya uanagenzi na vijana 22,296 wametambuliwa na kurasimishiwa ujuzi walioupata kupitia mfumo usiyo rasmi," alisema.

Alisema hatua nyingine ni kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007, kuwekeza zaidi katika sekta ya elimu iliyo bora, kuendelea kutoa elimu ya msingi na sekondari hadi kidato cha sita bila ada, kuendelea kuboresha bajeti ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

Pia, alisema serikali imeboresha mwongozo wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na kupata mwongozo mpya wa mwaka 2022 ambao miongoni mwa mambo yaliyoboreshwa ni fursa ya kijana kuweza kukopa, ongezeko la kiwango cha kukopa kutoka Sh. milioni 10 hadi Sh. milioni 50.

Alieleza kuwa kupitia mwongozo huo, Katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana umeweza kutoa mikopo ya Sh.bilioni 1.88 kwa miradi ya vijana na kwa mwaka huu mikopo ya Sh. bilioni 1.3 imetolewa.

Alisema kutoa mafunzo na elimu ya stadi za maisha kupitia programu ya stadi za maisha kwa vijana kwa lengo la kuhakikisha wanajitambua na wanaweza kukabiliana na kero maisha.

# Wakulima wahimizwa kuchangamkia zabibu zilizokaushwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA.

WAKULIMA wa zabibu wametakiwa kuchangamkia fursa zilizoko kwenye zabibu za kukausha ili kujiinua kiuchumi.

Mratibu wa Taifa wa Programu ya Utafiti wa Zabibu kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Makutupora, Saada Hussein aliyasema hayo juzi kwenye maonesho ya Nanenane Kanda ya Kati katika viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma.

Alisema zabibu hizo zina soko kubwa la ushindani ndani na nje ya nchi na zina faida kubwa kutokana na kwamba mkulima anaweza kuuza mvinyo ghafi katika viwanda vya kutengeneza vinywaji aina mbalimbali.

Alisema wameshatoa teknolojia za mbegu bora kwa ajili ya kilimo cha zabibu ambazo zimethibitishwa na Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu Nchini (TOSCI) kwa ajili ya kuanza kutumika na kusisitiza kuzitumia kwa kuwa zinatija.

Alibainisha wanaendelea kutoa elimu kwa wakulima mbalimbali kufanya kilimo chenye tija ambacho kitawasaidia kuwainua kiuchumi na kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

Alisema ili kuongeza uzalishaji wenye tija wakulima wanapaswa kuangalia eneo analolima lakini pia kufuata kanuni bora za kilimo hicho zinazotolewa na wataalamu wa kilimo.

Saada alitoa wito kwa wakulima kufuata kanuni za kilimo bora ili kupata tija na wale ambao hawajaingia katika kilimo cha zabibu waingie katika kilimo hicho.

Naye, mkulima wa zao hilo, Julius Eliud, aliishukuru TARI kwa jitihada inazofanya kwenye kilimo cha zabibu ambazo zinawasaidia wakulima kupiga hatua.

# 'Waajiri wekeni mazingira kuwasaidia kinamama kunyonyesha'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAAJIRI nchini wamehimizwa kuweka mazingira wezeshi yatakayowasaidia kinamama kunyonyesha watoto wao wakiwa kwenye maeneo yao ya kazi.

Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala wa Wizara ya Afya, Issa Ng'imba aliyasema hayo jana akifungua kikao cha waajiri kutoka sekta mbalimbali za umma na binafsi chenye lengo la kujadili namna bora ya kuweka mazingira wezeshi ya unyonyeshaji.

Alisema ili wanawake wanyonyeshe vizuri na kwa wakati watoto wao ni vyema kutenga vyumba maalumu mahala pa kazi ili mtoto atakapoletwa mama awe na uhuru wa kumnyonyesha mwanae bila kuwa na hofu au mwingiliano wa watu wengine.

"Unyonyeshaji wa mtoto kutoka anapozaliwa hadi anapofikisha siku 1,000 ni muhimu katika ukuaji wake na katika kipindi hiki anatakiwa kunyonya maziwa ya mama pekee ili kukua na kujenga mwili wake ikiwemo kinga dhidi ya magonjwa hivyo basi kwa kinamama wanaofanya kazi ni muhimu waajiri wao wakatenga maeneo maalum ya unyonyeshaji," alisema.

Aidha, Issa alibainisha kuwa maendeleo ya mtoto yanategemea ukaribu na mama yake ambaye anamnyonyesha kwani maziwa ya mama yana virutubisho vyote muhimu ambavyo mtoto anahitaji na anatakiwa kunyonya muda wote na sio kupangiwa ratiba.

Alisema kuwa Wizara Afya kwa kushirikiana na wadau pamoja na taasisi mbalimbali wana jukumu la kuendelea kutoa elimu kwa waajiri wa sekta rasmi na zisizo rasmi kutenga maeneo hayo ikiwamo sehemu ya watoto kucheza na kupumzika mara baada ya kunyonya.

Naye, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Lishe wa wizara hiyo, Neema Joshua alisema kauli mbiu ya mwaka huu imelenga kuona namna gani waajiri wanaweza kuweka mazingira wezeshi ya kuwawezesha kinamama kunyonyesha watoto wao akiwa kazini.







Wafanyakazi wa Benki ya Afrika Tanzania, wakizungumza na baadhi ya wateja waliotembelea banda la benki hiyo katika maonyesho ya wakulima Nanenane kitaifa katika viwanja vya John Mwakangale, jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Hospitali Kanda ya Mbeya yaanza ujenzi wodi ya upasuaji moyo, ubongo, mishipa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HOSPITALI ya Rufani Kanda ya Mbeya, imeanza mchakato wa kujenga jengo maalumu kwa ajili ya wodi ya upasuaji wa moyo, ubongo na mishipa ya damu kwa lengo la kuwasogezea wananchi huduma hizo ambazo kwa sasa hazipatikani.

Wananchi wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wanaohitaji huduma hizo kwa sasa wanalazimika kusafiri kwenda mkoani Dar es salaam katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na kwenye hospitali zingine ambako huduma zinapatikana.

Mkurugenzi Mtendaji wa hospitali hiyo, Dk. Godlove Mbwanji aliyasema hayo juzi alipokuwa anapokea msaada wa mifuko 610 ya saruji kutoka kwa mmoja wa wafanyabiashara wa vifaa vya ujenzi wa Jiji la Mbeya kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo.

Alisema hospitali hiyo kwa sasa inapokea idadi kubwa ya wagonjwa wanaohitaji huduma hiyo lakini wamekuwa wakilazimika kupatiwa rufani kwenda Dar es salaam na kwamba baadhi yao wamekuwa wakipata madhara zaidi.

"Tumekuwa tukipokea wagonjwa wa moyo zaidi ya 20 kila mwezi ambao tumekuwa tukilazimika kuwapatia rufani ili wasafiri kwenda Dar es salaam, lakini baadhi yao wamekuwa wakipoteza maisha kutokana na matatizo haya," alisema Dk. Mbwanji.

Hata hivyo alisema walilazimika kuanza ujenzi wa jengo hilo jipya kwa sababu hospitali ina uhaba wa majengo kutokana na kupandishwa hadhi kutoka kuwa ya mkoa mpaka kuwa ya kanda ikiwa na majengo yaleyale.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi wa jengo hilo, Dk. Dino Mwaja alisema wanakusudia kujenga majengo mawili kwa ajili ya huduma hizo ambayo moja litakuwa na vyumba viwili vya upasuaji wa moyo na ubongo na kimoja kwa ajili ya kulaza wagonjwa mahututi.

Alisema jengo lingine litakuwa kwa ajili ya upasuaji wa mishipa ya damu iliyoziba kwa maelezo kuwa huduma hiyo pia inahitaji chumba cha kujitegemea.

Dk. Mwaja alisema ili kukamilisha ujenzi wa majengo hayo wanahitaji zaidi ya Sh. bilioni 1.2 ambazo wanatarajia kuzipata kutoka kwenye vyanzo mbalimbali ikiwemo mapato ya ndani ya hospitali, michango ya wadau pamoja na serikali.

Akizungumza wakati wa kupokea msaada huo wa mifuko ya saruji, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Akson aliahidi kuchangia matofali yote 9,000 ambayo yanahitajika kwa ajili ya kazi hiyo.

Dk. Tulia alisema atachangia matofali hayo kwa awamu mbalimbali kulingana na namna ujenzi utekavyokuwa unaendelea mpaka utakapokamilika.

Aidha, alimshukuru mdau aliyechangia ambaye ni Wambura Maseke kwa mchango alioutoa akieleza kuwa ni mchango mkubwa ambao utasaidia kuharakisha mradi huo.

Akikabidhi sehemu ya mifuko hiyo ya saruji, mwakilishi wa mdau huyo ambaye ni Deusdedith Maseke alisema kaka yake aliamua kutoa mchango huo kwa sababu yeye ni miongoni mwa wanufaika wa huduma za afya katika hospitali hiyo.

Alisema pamoja na mchango huo, pia ataendelea kusambaza vifaa vya ujenzi kwenye hospitali hiyo ili aendelee kulipwa kidogo kidogo kwa awamu.

## TARI yabaini ufuta unatibu ugonjwa wa fangasi, bakteria

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Kituo cha Naliendele kilichopo Mtwara kimebaini ufuta unaweza kutibu tatizo la ugonjwa wa fangasi na magonjwa ya bakteria yanayowakabili wananchi.

Katika utafiti huo imebainika kuwa zao hilo limeweza kuongezwa thamani na kutengenezea mafuta ya kujipaka ambayo yanamaliza tatizo hilo la fangasi na bakteria.

Akizungumza na Nipashe mkoani Mbeya, Mratibu wa Programu ya Ufuta Kitaifa kutoka (TARI), Naliendele Joseph Nzunda, alisema tayari walianza kutumia kutokana na magonjwa hayo wamepona.

Nzunda alisema umuhimu wa mafuta hayo unatokana na ukweli kuwa ndani ya ufuta kuna kemikali na virutubisho mbalimbali pamoja na Vitamin E.

"Siyo magonjwa ya fangasi lakini bidhaa hiyo inatumika katika kutunza ngozi kwa sababu ndani ya ufuta kuna kemikali mbalimbali, Vitamin E na virutubisho mbalimbali" alisema

Alisema kama kauli mbiu ya maonesho haya kwa mwaka huu inavyosema 'Vijana na wanawake ni msingi Imara wa mifumo endelevu ya chakula' imekwenda na uhalisia kwa kuwa vijana na wanawake ni watumiaji wa zao hilo katika kuongeza mnyororo wa thamani kwa kutengeneza bidhaa mbalimbali. Maliam Masige mkazi wa jijini Mbeya ambaye alitembelea maonyesho Banda la Taasisi ya TARI kwenye maonesho hayo alisema yeye ni mmoja wa mashuhuda waliweza kutumia mafuta hayo ya ufuta kwa kumaliza tatizo la ngozi ambalo lilikuwa likimsumbua kwa muda mrefu baada ya kununua katika maonyesho ya mwaka 2022.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk Geofrey Mkamilo, alisema taasisi hiyo sio tu inazalisha teknolojia za mbegu za kisasa kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali lakini baadhi ya mbegu hizo kama ufuta, mtama, mihogo na jamii ya matunda pamoja na mikunde imekuwa pia ikitumika kwa ajili ya kutatua changamoto za afya ya binadamu.

# Elimu matumizi ya ardhi yatolewa kupunguza migogoro

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imesema imeongeza utoaji wa elimu ya matumizi sahihi ya ardhi ili kupunguza migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikiibuka katika maeneo mbalimbali nchini na wakati mwingine kuhatarisha hali ya amani.

Aidha, imesema katika usuluhishi wa migogoro nchini, imepokea malalamiko mengi zaidi yanayohusu migogoro ya ardhi kuliko migogoro mingine hali iliyoilazimu kuongeza kasi ya utoaji wa elimu kwa wananchi.

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Sara Mwaipopo aliyasema hayo jana alipozungumgza na waandishi wa habari jijini Mbeya ambapo alisema kumekuwa na ongezeko la mwitikio wa watu kupeleka malalamiko hayo kwenye ofisi za serikali.

Mwaipopo alisema katika utafiti wao walibaini kuwa migogoro ya ardhi imeongoza kupokelewa maeneo mengi nchini ambayo imefunguliwa dhidi ya serikali hali ambayo imewalazimu kutoa elimu zaidi.

"Tuna ofisi 17 Tanzania Bara na katika utafiti wetu tumeona kesi nyingi zinazopelekwa huko migogoro ya ardhi ndio inaongoza, lakini pia tumekuwepo kwenye maonyesho ya Nanenane na tumepokea watu wengi ambao wameleta malalamiko yao," alisema Mwaipopo.

Alisema hata kwenye maonyesho ya Nanenane walipokea malalamiko mengi zaidi yanayohusu migogoro ya ardhi hivyo wanakusudia kuishauri serikali njia ya kukabiliana na migogoro hiyo.

Alisema kwa sasa Tanzania imejikita kuangazia suala la usalama wa chakula, hivyo uwepo wa migogoro mingi ya ardhi inaweza kuathiri usalama na uzalishaji wa chakula hali inayowasukuma kuongeza kasi ya utoaji elimu na kuhakikisha migogoro yote ya ardhi inaisha kwa wakati.

Aliongeza kuwa wataendelea kuwepo kwenye Uwanja wa John Mwakangale mpaka muda wa siku saba uliotolewa na Rais Samia utakapomalizika baada ya kupokea ombi kutoka kwa Mbunge wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson

Aidha, alibainisha kuwa lengo la serikali ni kuhakikisha watu wanajikita kwenye shughuli za uzalishaji hivyo wao wamejikita kutatua mashauri hayo kabla hayajafika mahakamani.

Wakati wa kufunga maonyesho ya wakulima ya kimataifa (Nanenane) yaliyofanyika jijini Mbeya, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo alisema migogoro mingi ya ardhi nchini imekuwa ikisababishwa na baadhi ya wafugaji ambao wamekuwa wakiingiza mifugo kwenye maeneo wasiyoruhusiwa.

Alisema baadhi ya maeneo wafugaji hao wamekuwa wakichunga mifugo kwenye mashamba ya wakulima na hivyo kusababisha migogoro ambayo inahatarisha amani.

Hata hivyo wakati wa kufunguliwa kwa maonyesho hayo, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango aliwaagiza wakuu wa mikoa kushirikiana na Wizara ya Mifugo kuiondoa mifugo kwenye maeneo ambayo wamevamia na kuwapeleka kwenye maeneo yaliyotengwa.

Alisema kwenye utatuzi wa migogoro hiyo, wafugaji wanatakiwa kushirikishwa na waandaliwe mazingira rafiki ya kufugia ikiwemo kujenga malambo ya kunyweshea mifugo.



# Utendaji vikosi maalum wamkosha M/kiti Kamati Baraza la Wawakilishi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya viongozi wakuu wa kitaifa, Machano Othman Said, amesema utendaji kazi wa vikosi maalumu vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar umejenga sifa na uaminifu katika kusimamia miradi ya maendeleo na kiuchumi ya serikali.

Aliyasema hayo Zanzibar wakati akiwaongoza wajumbe wa kamati hiyo walipotembelea miradi inayotekelezwa na idara maalumu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika ujenzi wa miradi ya serikali pamoja na wapiganaji.

Alisema wajumbe wa kamati hiyo, wamefurahishwa na kazi nzuri inayofanywa na idara maalumu SMZ katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa ufanisi na ubora.

Machano alisema Serikali ya Zanzibar imetoa Sh.bilioni 28 kwa ajili ya kuvipatia vikosi vyake kutekeleza miradi ya ujenzi wa masoko yaliyopo Unguja na Pemba ambayo yatafungua milango kwa wajasiriamali kutekeleza majukumu ya kibiashara.

Mkuu wa JKU, Kanali Makame Abdalla Daima, alisema wamejipanga kutekeleza mradi wa ujenzi wa soko hilo lenye ghorofa mbili kwa kuzingatia viwango na ubora wake. Alisema wanatarajia kukamilisha kwa wakati na hivyo kutoa nafasi kwa wafanyabiashara kuendelea na shughuli zao kwa ufanisi mkubwa.

Naye Kamanda wa Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM), Azani Hassan Msingiri alisema wanatekeleza miradi inayotokana na fedha za UVIKO -19 ambayo wameifanya kwa ubora na ufanisi unaozingatia viwango.

Alisema wanaendelea na ujenzi wa kiwanda cha kusanifu na kuongeza bidhaa za mwani eneo la Chamanangwe Pemba ambapo ujenzi wake umefikia asilimia 90.

Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Mtumwa Peya Yussuf alisema vikosi vya idara maalum SMZ watendaji wake wameonesha ubunifu katika uzalishaji na hivyo kuongeza mapato ya serikali.

Alisema kikosi cha KMKM kimeonesha kwa vitendo utayari wa kutekeleza sera ya uchumi wa buluu katika uvuvi wa Bahari Kuu pamoja na ufugaji wa matango bahari na ufugaji wa samaki kwa kutumia meli inayokwenda katika maji yenye kina kirefu.



Kaimu Naibu Katibu Mkuu Zanzibar ambaye pia ni Katibu wa Habari na Uenezi Chama cha ACT Wazalendo, Salim Biman (kulia), akiwa na ujumbe wa chama hicho katika kikao cha pamoja na ujumbe wa Msajili wa Vyama vya Siasa nchini uliongozwa na Msajili Msaidizi, Hollo Kazi katika Ofisi Kuu ya ACT, Vuga Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ujenzi kiwanda cha mwani wafikia asilimia 90

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Uvuvi na Uchumi wa buluu imesema ujenzi wa kiwanda cha mwani eneo la Chamanangwe Pemba kimefikia asilimia 90, kwamba kitasaidia wakulima na kuongeza uzalishaji katika usarifu na thamani ya zao hilo.

Hayo yalisemwa na Katibu Mkuu Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Buluu, Aboud Suleiman Jumbe alipotembelea wakulima katika maonesho ya Nanenane.

Alisema kuelekea uchumi wa buluu kilimo cha mwani kimepewa kipaumbele cha kwanza kwa ajili ya kuwainua wakulima wake ambao kwa asilimia 80 ni wanawake waliopo vijijini Unguja na Pemba.

Jumbe alisema mradi wa ujenzi wa kiwanda cha mwani ambacho kinajengwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni mkombozi na kitasaidia kuleta mageuzi ya uzalishaji wa mwani kwa kuongeza thamani ya matumizi yake.

Alisema Shirika la Maendeleo la Korea KOICA wanatarajia kujenga kiwanda ambacho kitatokana na bidhaa zinazozalishwa na mwani kwa ajili ya matumizi ya ziada ikiwemo sabuni na manukato.

Aidha, alisema hizo ni baadhi ya juhudi zinazochukuliwa na serikali ya kuona kwamba ifikapo mwaka 2025 kwa asilimia 60 pato la taifa litatokana na uchumi wa buluu.

Jumbe alisema pia tayari kampuni ya mwani inayomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanza ununuzi wa bidhaa hiyo kutoka kwa wakulima ambapo bei imeongezeka kutoka Sh.500 iliyokuwa ikinunuliwa awali hadi Sh. 2,000.

Alisema matarajio makubwa ya bei ya mwani kufikia Sh.3,000 katika muda mfupi hatua ambayo ni mageuzi makubwa yanayofanywa na serikali katika kuwawezesha wakulima wa mwani kwenda na bei ya wakati uliopo sasa.

Naye Ofisa Mdhamini wa Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Buluu Pemba, Dk. Salum Mohamed Hamza, alisema wananchi wa Pemba wamehamasika na kuongeza juhudi za kulima mwani.

# Kampuni yajinasibu kuzalisha bidhaa zenye ubora

**Na Mwandishi wetu**

KATIKA kuboresha soko la biashara ya viywaji nchini, wazalishaji wa sharubati za ceres necta wanatarajia kuziba pengo kwenye usambazaji wa bidhaa zenye ubora.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa safu ya vinywaji vya ceres nectar vilivyofayiwa maboresho hivi karibuni, Mkuu wa Kitengo cha Mauzo na Masoko wa Leostar International Ltd, Chesco Mwapelwa, alisema watahakikisha Watanzania wanapata bidhaa bora na kwa bei nafuu sokoni.

Alisema pia wamezingatia maoni ya wateja wao na wanaamini kuwa bidhaa hizo mpya zitafanya vizuri sokoni.

Kiongozi wa Biashara ya Vinywaji ya PepsiCo kwa Afrika Magharibi, Mashariki na Kati, Isabel Coetzer, alisema juisi hizo zimekuwa sehemu muhimu ya maisha ya Watanzania katika miongo miwili iliyopita.

Meneja Masoko wa Pepsi-Co kwa vinywaji, Afrika Magharibi, Mashariki na Kati, Karen Veysey, alisema safu iliyofanyiwa maboresho imeendelezwa kwa msingi wa utafiti wa kina kuhusu Wateja.

“Utafiti huu ulitupa ufahamu kuhusu mapendekezo, mahitaji na tamaa za wateja. Mojawapo ya ufahamu muhimu ulikuwa kuwa wateja walikuwa wanatafuta juisi yenye muundo mzito zaidi na ladha ya matunda yenye nguvu, tamu na ya kuvutia zaidi,” alisema.

Alisema bidhaa hizo zinapatikana katika Ladha tano kwenye ukubwa tofauti ikiwamo ndizi, embe na matunda ya pesheni. caribbean crush ambayo ni mchanganyiko wa mananasi, ndizi, nazi, na topeo.

Alisema pia kuna multi fusion ambayo ni muunganiko wa kuvutia wa ndizi, nanasi, tofaa, machungwa na matunda ya parachichi.

# Kigogo CCM ataja siri ya kukijenga, kukiimarisha chama

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri ya CCM, Hemed Suleiman Abdullah amesema nguzo pekee ya kukijenga na kukiimarisha chama hicho ni umoja na mshikamano na viongozi kushirikiana katika kuwatumikia wanachama na wananchi. Aliyasema hayo katika muendelezo wa ziara yake ya kichama visiwani Zanzibar na kuwataka viongozi kuhakikisha wanatenda haki, usawa, ukweli na uwazi katika kukijenga chama.

Alisema kuna makundi ya wapambe katika chama yanayobeba viongozi na wagombea ambapo ni vyema kuungana na kuacha kujenga mgawanyiko.

Hivyo, aliwataka viongozi watumie ujuzi na nguvu zao katika kuunganisha wanachama kukiendeleza chama badala ya kuwagawa.

Aidha, aliwataka viongozi wa ngazi mbalimbali katika chama kujitahidi katika kusajili wanachama wapya, kusimamia wanachama kulipa ada kwa wakati na kupatiwa kadi za kieletroniki. Alisema CCM kitaendelea kutekeleza ilani yake kwa kuijenga Zanzibar kiuchumi na kutatua, kutekeleza ahadi zake kivitendo.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mjini, Talib Ali alisema kuna viongozi wa vyama vya upinzani wanapotosha umma wa Wazanzibari kwa kuichafua serikali na kuwasihi wanachama wa CCM kueleza mazuri yanayofanywa na viongozi wanaopenda maendeleo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Mjini, Rashid Simai Msaraka alisema ziara hiyo ya Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa ni ya mafanikio ambapo inadhihirisha utayari wa viongozi wakuu wa serikali katika kukiimarisha chama. Alisema kwa mujibu wa ilani ya uchaguzi ya chama hicho ya mwaka 2020-2025 tayari utekelezaji wake umekamilika kwa asilimia 100 kwa kuzingatia sekta mbalimbali ikiwemo michezo, elimu, maji na miundombinu.

Katika ziara hiyo pamoja na mambo mengine aliweka jiwe la msingi ujenzi wa Tawi la CCM Nyerere ‘A’ pamoja na kukabidhi hati ya nyumba iliyonunuliwa kwa ajili ya ujenzi wa Tawi la CCM Meya Bondeni.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA PASSPORT



COSTANTINA BARNABA Mtajwa hapo juu amepotelewa na passport yenye NO, TAE 259472 iliyotolewa na ofisi ya uhamiaji tarehe 11 Mwezi Dec mwaka 2019.
Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi BNG/RB/500/2023

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 81 OF 2023**
**In the Matter of the Estate of the Late: DIONIS SILVERY DIU**

**By 1. EMMANUEL JOHN MTESA**
**2. ……………………………………**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 24 day of 08/2023
Dated at MOROGORO this 28 day of 07..2023

……………………………………

**RESIDENT MAGISTRATE**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ROGASIANI GERALD MADAULA** Anatangaza kupotelewa na kadi ya piki piki yenye namba za usajili MC 146 CRN(FEKON) Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi **MOR/RUH/B/241808/2023.**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



RAHMA MSAFIRI SAILOS anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba: S.1022-0087 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia KAMBANGWA SECONDARY SCHOOL mwaka 2018. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .
POLISI TAARIFA: DAR/MAG/RB/101909/2023

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MATHIAS ANDREW MASSAE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba: T 861 ACH kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**KW/RB/3043/23**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SAHURI LA MADAI NAMBARI 160 LA 2023**
**LUCY BERNARD CHARKES MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**
- **MICHAEL GREGORY**

**5. ERASMUS HIMILI**
- **BAKARY MHANDO**

**6. DANIEL MATHIAS MDAIWA/WADAIWA**
- **MUDY**

**7. THEO ELEOTELY**
- **ZUHURA MOHAMEDI**

**WITO KUITWA SHAURINI**
- **MICHAEL GREGORY**

**. MUDY**
**7. ERASMUS HIMILI**
- **BAKARI MHANDO**

**4. ZUHURA MOHAMEDI**
- **DANIEL MATHIAS**

**6.THEOELEOTELY**

**POPOTE ULIPO/MLIPO**

LUCY BERNARD CHARLES amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni ( Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 04/09/2023 saa tatu asubuhi/mchana mbele ya Mh. J.W. SILLAS Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 10 Mwezi 08 ,2023

---

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Baraza jipya la mawaziri latangazwa Niger

**NIAMEY,** Niger

KIONGOZI wa serikali ya kijeshi ya Niger Jenerali Abdourahmane Tchiani ametangaza baraza lake la mawaziri.

Hatua hiyo ni sawa na kwenda kinyume na wito wa viongozi wa nchi za Afrika Magharibi ambao wanataka kurejeshwa madarakani Rais aliyepinduliwa Mohamed Bazoum.

Baraza hilo la mawaziri lilitangazwa jana kupitia runinga ya serikali, saa sita na nusu kwa saa za nchi hiyo. Serikali mpya inaundwa na mawaziri 21, wakiwemo manaibu waziri na mjumbe wa waziri.

Serikali hiyo mpya ya mpito, inayoundwa na wanajeshi na raia, inaongozwa na Waziri Mkuu wa muda Lamine Zeine Ali Mahamane, ambaye pia atahudumia kama waziri wa uchumi na fedha.

Aliyekuwa mkuu wa wafanyakazi Luteni Jenerali, Salifou Mody, anayechukuliwa kama naibu wa Jenerali Tchiani, ameteuliwa kuwa waziri wa ulinzi wa taifa.

Kanali Maj Abdourahmane Amadou, ambaye amekuwa akisoma taarifa nyingi kwenye runinga ya serikali tangu mapinduzi ya Julai 26, ni waziri wa vijana na michezo.

Tayari jeshi hilo limewataja wakuu wapya wa kijeshi na kuwafuta kazi maofisa wengi wakuu wa serikali waliohudumia katika utawala wa Bazoum.

Wakati huo huo, Marekani na Umoja wa Mataifa zinatilia shaka hali ya kiafya na kiusalama ya Rais aliyeondolewa madarakani Mohamed Bazoum. Kiongozi huyo amewekwa kizuizini tangu kufanyika kwa mapinduzi hayo.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres pia alisema ana wasiwasi huo kutokana na hali mbaya ya maisha ambayo familia hiyo inayapitia.

Bazoum aliondolewa madarakani tarehe 26 Julai, baada ya walinzi wake kuipindua serikali yake. **BBC**

# Museveni atoa kauli uamuzi Benki ya Dunia kwa Uganda

**Na Maulid Mmbaga**

HUKU Rais Yoweri Museveni akisema Uganda inaweza kujiendesha na kupiga hatua kimaendeleo bila mikopo, wanadiplomasia na wachumi wamesema uamuzi wa Benki ya Dunia (WB), kusitisha utoaji mikopo kwa Uganda, uziamshe nchi za Afrika zijiimarishe kiuchumi.

Wataalamu hao waliiambia Nipashe jana kuwa kinachotokea Uganda ni fundisho kwa Afrika hasa katika kuwa na mkakati wa kujitegemea kiuchumi, kukataa baadhi ya masharti kabla ya kutia saini mkataba wowote.

Juzi, WB ilitangaza kusitisha utoaji wa mikopo mipya kwa serikali ya Uganda baada ya Rais Museveni kutia saini muswada wa sheria inayokataza wanaoshiriki mapenzi ya jinsia moja, kwamba inakinzana na maadili ya benki hiyo.

Inaelezwa kuwa hadi mwishoni mwa 2022, WB ilitoa zaidi ya dola bilioni 5.4 kufadhili miradi ya maendeleo katika sekta za afya na elimu inayotajwa huenda ikaathiriwa na uamuzi mpya wa benki hiyo.

**...Afrika inahitajika lakini bado haijajua namna ya kuchanga karata zake vizuri. Afrika iamke ianze kujitegemea, na elimu zaidi inahitajika kutolewa.**

Mhadhiri katika Chuo cha Taifa cha Diplomasia, Abbasi Mwalimu, alisema kinachoendelea Uganda ni athari ya moja kwa moja kidiplomasia.

Alisema jambo hilo linapaswa kuchukuliwa kama fundisho kwa nchi za Afrika ili zijiwekee utaratibu wa kujitegemea, hasa kwa kutumia fedha za ndani katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati inayogusa sekta nyeti, pamoja na kuondokana na kasumba ya utegemezi.

Alisema kitendo cha baadhi ya mataifa makubwa kuishinikiza Uganda kukubali suala la mapenzi ya jinsia moja siyo sawa, huku akisisitiza mataifa ya Afrika kuongeza uzalishaji na kukuza mzunguko wa biashara ndani ya Afrika, kwa kuwa itasaidia kuepukana na changamoto zinazoikabili Uganda kwa sasa.

Alisema kuna haja ya nchi za Afrika kuacha kutegemea misaada, akisema "...Afrika inahitajika lakini bado haijajua namna ya kuchanga karata zake vizuri. Afrika iamke ianze kujitegemea, na elimu zaidi inahitajika kutolewa. Benki ya Afrika iweke mikakati kila nchi ya Afrika iweke fedha na kuziwezesha kupata mikopo rafiki na kuepuka ile yenye masharti ya tofauti."

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti wa Kuondoa Umaskini (REPOA), Dk. Donald Mmari, alishauri nchi za Afrika kujiimarisha kiuchumi na mifumo ya ndani ya ukusanyaji kodi ili watekeleze miradi kwa fedha zao.

Kwa mujibu wa Dk. Mmari, takwimu zinaonyesha kuwa ukusanyaji wa kodi kwa mataifa ya Afrika uko chini ya asilimia 20 tofauti na mataifa mengine, ambayo ukusanyaji ni juu ya asilimia 30, huku akisisitiza mifumo imara ya ukusanyaji wa mapato ya ndani itasaidia taifa



Raia wa Cuba wakiogelea katika dimbwi la maji karibu na ufukwe wa mji mkuu wa Havana baada ya wakazi wake kukabiliwa na hali ya joto kali, na kusababisha kukimbilia kujipoza mwili kwenye mabwawa ya asili yaliyojengwa na familia tajiri katika nusu ya kwanza ya karne iliyopita. **PICHA: AFP**

# Bibi adaiwa kumchoma mjukuu kisa wizi 2,000/-

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MTOTO wa darasa la kwanza katika Shule ya Msingi Boko Mnemela, wilayani Kibaha, anauguza majeraha ya viganja vyake vya mikono vilivyoungunzwa kwa moto na bibi yake kwa madai ya kumwibia Sh. 2000.

Ni wiki mbili sasa tangu tukio la kuunguzwa viganja vyake litokee, kutokana na kufanyiwa kitendo hicho na bibi yake ambaye ni mpika vitumbua.

Mmoja wa majirani wa mtoto huyo ambaye ameomba kuhifadhiwa jina lake, alisema alipata taarifa kutoka kwa mtu wake wa karibu ambaye alimueleza kuhusiana na tukio la mtoto huyo.

Alisema taarifa hizo alizipata usiku na siku iliyofuata asubuhi, alikwenda nyumbani anakoishi mtoto huyo na kumkuta akiwa anacheza na rafiki zake huku akiwa na tahadhari ya mikono yake.

Baada ya kufika, alisema alimwita na kumuuliza nini kimetokea ndipo akamwaleza kwamba ni wiki mbili tangu achomwe na moto kwenye viganja vya mikono yote miwili na bibi yake anayemlea.

Jirani huyo alisema siku ya tukio, bibi huyo alimtuhumu mjukuu wake kuiba Sh. 2,000 ndipo alipochukua majani makavu na kuyafunga kwa kamba kwenye kiganja chake na kisha kuwasha moto.

Alipojaribu kuwauliza majirani wa karibu kuhusiana na taarifa za mtoto huyo, walisema walikuwa wanajua kilichotokea lakini waliogopa kutoa taarifa kwenye vyombo vya sheria kwa kuhofia uhasama.

Baada ya hapo, alisema aliondoka na mtoto huyo na kwenda naye hadi kwa mwenyekiti ambaye walimfuata bibi aliyekuwa anaendelea na biashara yake ya vitumbua na alipoulizwa alisema majeraha hayo yalitokana na mtoto kuangukia kwenye moto.

Alisema waliondoka na mtoto huyo kwenda Kituo cha Polisi Mji Mdogo na baadaye kumpeleka Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Tumbi kwa matibabu lakini hawakufanikiwa kwa sababu hawakuwa na fedha.

Juzi walimpeleka tena Tumbi kuanza matibabu huku ndugu wa upande wa mtoto huyo wakilaumu kitendo cha kesi hiyo kufikishwa polisi.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mnemela Kibaoni, Michael Mwinza, alithibitisha kuwapo kwa tukio hilo la mtoto kuchomwa moto viganja vyake ambalo alisema alipata taarifa kutoka kwa mmoja wa wananchi wa eneo lake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Kamishna Msaidizi (ACP) Pius Lutumo, alisema mtuhumiwa Asna Mohamed (62), anashikiliwa kwa tuhuma za kumjeruhi mjukuu wake huyo ambaye anaishi naye tangu akiwa na umri wa mwaka mmoja.

Kamanda Lutumo alisema mtoto huyo amejeruhiwa kwenye viganja vya mikono yake miwili kwa kuchomwa moto kwa madai ya kuiba Sh. 2,000 na sasa anaendelea na matibabu katika hospitali ya Tumbi. Alisema mtuhumiwa atafikishwa mahakamani upelelezi ukikamilika.

Mkurugenzi wa Kituo cha Msaada wa Kisheria Kibaha (KPC), Catherine Mlenga, alisema bado tatizo ni kubwa kwenye eneo la ukatili unaofanywa kwa watoto.

"Baadhi ya matukio yanasababishwa na maisha magumu, hivyo mtoto akichukua hela kama hiyo mzazi au mlezi anachukua adhabu nzito kumwonya ambayo inaleta madhara," alisema.

Mlenga anashauri adhabu kali kwa watakaobainika kujihusisha na vitendo hivyo, ili iwe fundisho kwa wengine na kutokomeza vitendo hivyo kwa jamii.

Alisema kituo hicho kwa sasa kinaendelea kutoa elimu katika maeneo mbalimbali yakiwamo shuleni, minadani na nyumba kwa nyumba kwa lengo la kumaliza vitendo hivyo.

# JULIO AFUNGUKA SABABU ILIYOIBEBA YANGA TANGA

**Na Faustine Feliciane,** TANGA

BAADA ya kufanikiwa kutinga hatua ya fainali ya michuano ya Ngao ya Jamii, Kocha wa zamani wa Simba, Jamhuri Kihwelu 'Julio' amesema wachezaji wa Yanga wana 'kitu ndani' ambacho wanawazidi nyota wa timu nyingine hapa nchini.

**Akizungumza baada ya Yanga kuifunga Azam FC mabao 2-0, Julio alisema wachezaji wa timu hiyo wana uwezo wa kupata mabao dakika yoyote ya mchezo kutokana na namna wanavyopambana.**

Julio alisema wachezaji wa Yanga wana moyo wakujituma na kupambana muda wote wa mchezo na ndio sababu iliyowafanya waibuke na ushindi katika mchezo huo wa juzi na sasa wanajipanga kutetea taji wanaloloshikilia.

"Mimi nasemaga wazi, wachezaji wa Yanga wanajituma muda wote, ukiangalia mchezo wao na Azam, wao walionekana kabisa kuna kitu wanatafuta, walipambana muda wote na kweli wakafanikiwa kupata ushindi dakika za mwisho, wana ari ya kupambana zaidi ukilinganisha na wachezaji wa timu nyingine," alisema Julio.

Aliongeza wachezaji wote wa Yanga walicheza kwa kujituma na kuonyesha walihitaji matokeo chanya na kila mmoja akipambana kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

"Azam hawakuwa na utulivu hasa kipindi cha kwanza na robo ya mwisho ya mchezo, walikuwa wanacheza kwa fujo na ikawagharimu na kujikuta wanapoteza mchezo," alisema Julio.



Alisema Yanga walistahili kupata ushindi huo kutokana na utulivu na kujituma kwao hasa kipindi cha pili na kocha wao (Miguel Gamondi) alifanya mabadiliko sahihi ya wachezaji.

"Kipindi cha pili hasa katika eneo la kiungo, Yanga walikuwa na utulivu sana,walicheza kwa kujituma na kuwazima viungo wa Azam FC, kwangu mimi Yanga walistahili ushindi walioupata," alisema beki huyo wa zamani wa Simba na Taifa Stars.

Mabao ya Yanga katika mchezo huo wa nusu fainali ya kwanza ya Ngao ya Jamii uliochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini hapa yalifungwa na Stephano Aziz Ki na Clement Mzize.



Mdhamini wa Ligi ya Wilaya ya Iringa Mjini, Fadhil Ngajilo (kulia), akimkabidhi vifaa mbalimbali vya michezo kiongozi wa timu ya Africa Wondere's, Said Chitalula kwa ajili ya klabu 10 zitakazoshiriki ligi hiyo itakayoanza kesho mkoani Iringa. Wengine katika picha ni viongozi wa soka wa wilaya hiyo. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Aziz Ki: Nilifuata maelekezo

**Na Faustine Feliciane,** TANGA

NYOTA wa Yanga, Stephano Aziz Ki, amesema goli alilofunga katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya Ngao ya Jamii dhidi ya Azam FC hapo juzi lilitokana na yeye kufuata maelekezo ya kocha wake, Miguel Gamondi, imefahamika.

Aziz Ki alifunga bao la kwanza katika ushindi wa magoli 2-0 ambao Yanga waliupata na kutinga fainali ya michuano hiyo ya kufungua pazia la msimu mpya.

Nyota huyo alisema Gamondi alimtaka akabadilishe mchezo baada ya kuona dakika za lala salama zinakaribia na hakuna timu iliyopata bao lolote.

"Kocha kuna kitu aliona hakipo sawa katika safu yetu ya mbele, alinipa maelekezo na mimi nikayafanyia kazi, nashukuru tumepata ushindi, kocha wetu alikuwa na maono makubwa katika mchezo ule, tunashukuru sana tumepata ushindi ambao umetupa hamasa kubwa," alisema Aziz Ki.

Aliongeza mechi hiyo haikuwa nyepesi kwa sababu Azam pia walijitahidi kuwabana katika muda mwingi wa mchezo huo.

Alisema kwa sasa wanajipanga kwa ajili ya mchezo wa fainali na endapo wataibuka na ubingwa, watakuwa katika morali kubwa kuelekea kwenye michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Yanga ambao ni mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara wataanza msimu mpya kwa kucheza dhidi ya KMC Agosti 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi.



## Dabo awatoa hofu mashabiki wa Azam FC

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Yousouph Dabo, amesema bado ana muda wa kukijenga kikosi chake na anaamini kitafanya vizuri katika mechi za Ligi Kuu Bara na mashindano ya kimataifa watakayoshiriki.

Baada ya kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Yanga, Azam sasa inasubiri kucheza mechi ya kuwania mshindi wa tatu.

Dabo aliliambia gazeti hili matokeo ya mchezo huo wa juzi yamewaumiza lakini yamempa nafasi ya kubaini mapungufu na kuanza kuyafanyia kazi.

"Bado nina muda wa kurekebisha mambo, tumecheza mchezo mgumu dhidi ya Yanga na nimeona nini kinatakiwa kuongezwa katika kikosi changu, tumepoteza kwa sababu wenzetu Yanga walikuwa na wakati mzuri, nitazitumia vizuri siku zilizobaki kuakikisha tunakuwa sawa kuelekea kwenye ligi," alisema Dabo.

Licha ya kuanza kupoteza taji la kwanza, kocha huyo alisema bado mipango yake msimu huu ni kufanya vizuri zaidi ya msimu uliopita.

## Maxime: Tumejipanga kutoa dozi 2023/2024

**Na Adam Fungamwango**

ZIKIWA zimebakia siku chache kabla ya kuanza kwa msimu mpya, Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, amesema anaamini atafanya vyema katika Ligi Kuu Tanzania Bara kutokana na usajili mzuri waliofanya.

Akizungumza mara baada ya kuwasili kutoka Uganda walipokwenda kucheza mechi za kirafiki, Maxime alisema namna kikosi chake kilivyoimarika, anaamini atatetemesha kila timu watakayokutana nayo.

"Usajili ulienda vizuri na tumeshamaliza mambo hayo na tukaanza 'pre season', sasa tuna mwendelezo mzuri tu, na tupo tayari kwa ligi, unajua katika soka usiangalie sana usajili wa wenzako, angalia wewe mwenyewe umejipanga vipi kukabiliana na yoyote atakayekuja," alisema Maxime.

Aliongeza mechi nne za kirafiki walizocheza zimempa mwanga wa kikosi chake na hakuzingatia matokeo waliyopata.

"Tumecheza mechi nne za kirafiki, kwetu kipimo hicho kilikuwa kizuri sana kwa sababu ukipata timu za Kiganda ziko vizuri zinakusaidia kufahamu ubora wako," Maxime alisema.

HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

## PAVARD ANUKIA UNITED

KLABU ya Manchester United inatumaini kumuunganisha tena, Benjamin Pavard, mwenye umri wa miaka 27 na mchezaji mwenzake wa zamani wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Raphael Varane (30), kwa kutoa ofa ya euro milioni 30 kwa mlinzi huyo wa Bayern Munich. ***(L'Equipe)***

## AMRABAT ATAJWA UNITED

MANCHESTER United pia imeonyesha nia ya kumsajili, Sofyan Amrabat wa Fiorentina, huku raia huyo wa Morocco mwenye umri wa miaka 26 akipatikana kwa pauni milioni 30. ***(Mail)***

## NEYMAR, PSG KUJADILIANA

MAOFISA wa Paris St-Germain na mshambuliaji wa Brazil, Neymar, 31, watakutana wiki hii katika jaribio la kutatua mustakabali wa mchezaji huyo na kusitishwa kwa mkataba wake ni miongoni mwa masuala yatakayojadiliwa. ***(UOL Sport Brasil)***

## CAICEDO AKARIBIA CHELSEA

CHELSEA inakaribia kumsajili kiungo wa Ecuador, Moises Caicedo, mwenye umri wa miaka 21 kutoka Brighton na wana nia ya kukamilisha usajili kwa wakati ili acheze mchezo wa ufunguzi wa Ligi Kuu England dhidi ya Liverpool utakaochezwa keshokutwa. ***(Guardian)***

## KEPA ATAKIWA BAYERN

GOLIKIPA wa Chelsea, Kepa Arrizabalaga, mwenye umri wa miaka 28 anasakwa na kocha wa zamani wa The Blues, Thomas Tuchel, aliyepo Bayern Munich huku timu hiyo ya Bundesliga ikitafuta mbadala wa Mjerumani, Manuel Neuer (37), ambaye ameumia. ***(Fabrizio Romano)***

## LUKAKU MAMBO BADO

CHELSEA imeamua kusitisha mazungumzo na Juventus kuhusu mkataba wa kubadilishana unaomhusisha mshambuliaji wa Serbia, Dusan Vlahovic, mwenye umri wa miaka 23 na mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku (30). ***(Sky Sport Italia Via Football Italia)***

## RAYA KUZEEKEA ARSENAL

GOLIKIPA wa Brentford na Timu ya Taifa ya Hispania, David Raya, 27, anatazamiwa kujiunga na Arsenal kwa mkopo akiwa na chaguo la kujiunga moja kwa moja ifikapo msimu ujao. ***(Agthletic)***

## ARSENAL YAIGOMEA MONACO

ARSENAL wamekataa dau la pauni milioni 30 kutoka kwa Monaco inayoshiriki Ligue 1 kwa ajili ya mshambuliaji wao Mmarekani, Folarin Balogun, 22. ***(90min)***

## MAATSEN AGOMBEWA

WEST Ham inashindana na Burnley kwa ajili ya kumnasa kwa mkopo mlinzi wa kushoto wa Chelsea, Ian Maatsen, 21. ***(Mail)***

## FERNANDEZ KUTUA BURNLEY

KLABU ya Burnley pia inataka kumsajili beki wa pembeni wa Manchester United, Alvaro Fernandez, 20, kwa mkopo baada ya mchezaji huyo kuonyesha kiwango kizuri akiwa Preston katika msimu uliopita. ***(Sky Sports via Twitter)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE AENDELEA KUICHANGANYA PSG

**●●● Straika huyo sasa huenda akakosa mechi zote za Agosti...**

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappé hatahusika katika mechi ya ufunguzi ya Ligi Kuu Ufaransa maarufu Ligue 1 wakati Paris Saint-Germain itakapowakabili Lorient kesho kwenye Uwanja wa Parc des Princes, kwa mujibu wa ESPN.

**Mshindi huyo wa Kombe la Dunia mwaka 2018 hajafanya mazoezi na kikosi cha kwanza chini ya Kocha mpya, Luis Enrique huku kukiwa na mzozo wa mkataba na klabu hiyo.**

Kwa mujibu wa vyanzo vya ESPN, Mbappé anaweza kukosa kila mechi ya PSG mwezi huu ambazo zitakuwa ni dhidi ya Lorient, Toulouse na Lens kama adhabu.

Mbappé hivi karibuni aliiambia PSG hataongeza mkataba wake na alipanga kuondoka katika klabu hiyo kwa uhamisho wa bure ifikapo Juni, mwakani.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa aliachwa katika ziara ya PSG ya Japan kabla ya msimu mpya, huku Rais wa Klabu hiyo, Nasser Al-Khelaifi akidai ama akubali mkataba mpya zaidi ya Juni, 2024 au akubali kuondoka msimu huu wa joto.

Fowadi huyo amefanya mazoezi na wachezaji "wasiotakiwa" wakiwa njiani kuondoka PSG ambao ni pamoja na Leandro Paredes, Georginio Wijnaldum na Julian Draxler.

Al Hilal ndio klabu pekee iliyowasilisha ombi rasmi la kutaka kumnunua Mbappé, lakini endapo atahama, anataka tu kujiunga na Real Madrid.

Madrid wamekuwa wakimfuatilia Mbappé kwa zaidi ya muongo mmoja na walijaribu kumsajili katika kila dirisha la uhamisho wa majira ya joto mawili yaliyopita.

Vyanzo vimeiambia ESPN vigogo hao wa Ufaransa, PSG iko tayari kutomchezesha Mbappé katika kikosi cha kwanza kwa msimu mzima kama mchezaji huyo hatabadili mawazo yake.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,142,1

MECHI KALI
BURNLEY
VERSUS
MANCHESTER CITY
1 | 8.16
X | 4.93
2 | 1.38

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MAGUIRE RASMI MALI YA WEST HAM



**LONDON,** England

KLABU ya West Ham imekubali mkataba wa karibu pauni milioni 30 ili kumsajili beki wa Manchester United, Harry Maguire, vyanzo vimeiambia ESPN.

West Ham pia wamekubali dili la kiungo wa Southampton, James Ward-Prowse, anayelengwa kuchukua nafasi ya Declan Rice, ambaye alijiunga na Arsenal mwezi uliopita. Maguire mwenye umri wa miaka 30 amekuwa hapendezwi na United chini ya Kocha, Erik ten Hag, ambaye amewapendelea Raphaël Varane na Lisandro Martinez.

Mwezi uliopita alivuliwa kitambaa cha unahodha na kupewa Bruno Fernandes kama nahodha mpya wa klabu hiyo. ESPN iliripoti Jumatatu, United ilikataa ofa ya Maguire na Scott McTominay ya karibu pauni milioni 20, lakini West Ham walirudi na ofa nyingine.

West Ham bado hawajafikia dau la pauni milioni 40 la United kwa McTominay. Maguire alijiunga na Old Trafford kutoka Leicester City mwaka 2019 kama sehemu ya mpango wa pauni milioni 80 ambao ulimfanya kuwa beki ghali zaidi katika historia.

Hata hivyo, baada ya kuanza mara nane tu katika mechi za Ligi Kuu England msimu uliopita, United imekuwa tayari kusikiliza ofa za kumnunua beki huyo.

Maguire ambaye ameichezea England mechi 57, anahitaji muda wa kucheza ili kubakia katika mipango ya Kocha wa timu ya taifa, Gareth Southgate kwa ajili ya michuano ya euro 2024.



## Kessie kwenda Al Ahli ya Saudia

**BARCELONA,** Hispania

MCHEZAJI wa Barcelona, Franck Kessie, amejiunga na klabu ya Al Ahli ya Saudi Arabia, vigogo hao wa LaLiga wametangaza.

Al-Ahli atalipa euro milioni 12.5 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, ambaye alijiunga na Barca kwa uhamisho wa bure kutoka AC Milan mwaka jana.

Hata hivyo, kiungo huyo wa kati wa Ivory Coast hakuwa na nafasi katika kikosi cha kwanza cha Kocha, Xavi.

Klabu ya Al Ahli pia imemteua, Matthias Jaissle, kama kocha wa timu hiyo kwa kumpa mkataba wa miaka mitatu baada ya Red Bull Salzburg kumfukuza kocha huyo wa Ujerumani.

Kessie amekuwa mchezaji wa tano anayecheza Ulaya kujiunga na Al Ahli baada ya Riyad Mahrez, Roberto Firmino, mlinda mlango, Édouard Mendy na Allan Saint-Maximin.

Mfuko wa Uwekezaji wa Umma wa Saudi (PIF) umetangaza mradi wa uwekezaji na ubinafsishaji wa klabu za michezo unaohusisha mabingwa wa ligi hiyo, Al Ittihad, Al Ahli, Al Nassr na Al Hilal.

32,257/-

# SPORTPESA YAIMWAGIA NAMUNGO BILIONI MOJA

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya burudani na michezo ya ubashiri SportPesa, jana imeingia mkataba mpya wa kuendelea kuidhamini Namungo FC ya Lindi kwa kipindi kingine cha mwaka mmoja.

Waliohudhuria kutoka SportPesa ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Tarimba Abbas, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano, Sabrina Msuya na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Namungo, Omar Kaaya.

Akizungumza jijini jana, Tarimba alisema anayofuraha kutangaza SportPesa imefikia makubaliano na Namungo kuendelea kuwa mdhamini mkuu kwa kipindi kingine cha mwaka mmoja.

"Ninayo furaha kuwajulisha SportPesa tutaendelea kuwa wadhamini wakuu wa Namungo kwa kipindi kingine cha msimu 2023/24. Udhamini huu ni sehemu ya adhima yetu ambayo tumekuwa nayo katika kuunga mkono mpira wa Tanzania, tangu tumeanza rasmi shughuli zetu za kibiashara mwaka 2017, tumekuwa mstari wa mbele kuzishika mkono timu zetu kuliko kampuni yoyote ya ubashiri Tanzania," alisema Tarimba.

Alisema mkataba wa sasa wameboresha zawadi ambazo Namungo FC atakuwa anapata pale atakapokuwa anafanya vizuri. Kwa ufupi udhamini huu unaenda kuboresha ufanisi wa timu ya Namungo katika maeneo mbali mbali katika timu yao. Mfano endapo watashika nafasi nzuri katika ligi na mashindano mengine kama FA na CAF.

**Alisema mkataba huo mpya una thamani ya Sh. bilioni 1.055 na utamalizika ifikapo mwakani.**

Naye Kaaya aliwashukuru SportPesa kwa kukubali kuendelea kudhamini timu yao na anaahidi itatoa ushindani katika ligi.

"Hiki walichofanya leo (jana), cha kuendelea kutudhamini kwa mwaka mmoja inaonyesha imani yao kwetu, na pia itakuwa chachu kwa benchi la ufundi na wachezaji katika kuhakikisha nembo ya mdhamini inapata zaidi ya kile wanachostaili.

Niweke wazi SportPesa imekuwa na mchango mkubwa katika mafanikio yetu na pia katika ukuaji endelevu wa tasnia ya soka inayotuzunguka," Kaaya alisema.

Namungo ilimaliza msimu uliopita ikiwa katika nafasi ya tano, nyuma ya mabingwa, Yanga, Simba, Azam FC na Singida Fountain Gate.




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa SportPesa, Tarimba Abbas (kushoto), akimkabidhi jezi Ofisa Mtendaji Mkuu wa Namungo FC, Omar Kaaya baada ya kusaini mkataba mpya wa kuendelea kuidhamini timu hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Yanga: Skudu yuko poa



**Na Saada Akida,** TANGA

UONGOZI wa Yanga umesema afya ya kiungo wao mpya, Mahletse Makudubela 'Skudu' ambaye aliumia katika mechi ya hatua ya nusu fainali dhidi ya Azam FC iliyochezwa juzi, inaendelea vyema.

Kuumia kwa nyota huyo kulizua taharuki kwa mashabiki wa timu hiyo, baada ya kucheza dakika sita tu na nafasi yake kuchukuliwa na Crispin Ngushi.

Akizungumza na Nipashe jana, Daktari wa Yanga, Moses Etutu, alisema nyota huyo anaendelea vyema baada ya kufanyiwa vipimo alionekana hajavunjika na hivyo aliruhusiwa kurejea hotelini.

Kwa sasa atakuwa chini ya uangalizi na kutumia dawa za kupunguza maumivu, ninaimani kwa muda mfupi atakuwa sawa, mashabiki wasiwe na hofu juu ya nyota huyo," alisema Etutu.

Yanga itashuka tena dimbani keshokutwa kucheza mechi ya fainali dhidi ya Simba au Singida Fountain Gate FC.


## SUPA JACKPOT
## MECHI WIKI HII
### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 13/08/23 | 13:00 | Daejeon Citizen FC vs FC Seoul | 2.75 | 3.20 | 2.27 |
| 02. 13/08/23 | 13:30 | Incheon United FC vs Daegu FC | 2.25 | 3.10 | 2.80 |
| 03. 13/08/23 | 14:00 | Naestved BK vs Kolding IF | 2.75 | 3.25 | 2.23 |
| 04. 13/08/23 | 15:15 | FC Baden vs FC Vaduz | 2.65 | 3.20 | 2.33 |
| 05. 13/08/23 | 16:00 | IK Sirius vs Kalmar FF | 2.25 | 3.15 | 2.80 |
| 06. 13/08/23 | 16:00 | Brentford FC vs Tottenham Hotspur | 2.70 | 3.45 | 2.37 |
| 07. 13/08/23 | 16:00 | FC Nantes vs Toulouse FC | 2.46 | 3.30 | 2.70 |
| 08. 13/08/23 | 16:00 | Hobro IK vs Vendsyssel FF | 2.39 | 3.25 | 2.55 |
| 09. 13/08/23 | 17:00 | Cercle Brugge vs KRC Genk | 2.80 | 3.50 | 2.28 |
| 10. 13/08/23 | 17:00 | Motherwell FC vs Hibernian FC | 2.55 | 3.25 | 2.65 |
| 11. 13/08/23 | 18:00 | Burgos CF vs SD Huesca | 2.27 | 3.05 | 3.20 |
| 12. 13/08/23 | 18:00 | FF Jaro vs HIFK Helsinki | 2.55 | 3.20 | 2.42 |
| 13. 13/08/23 | 18:30 | Halmstads BK vs IFK Norrkoping FK | 2.55 | 3.10 | 2.46 |
| 14. 13/08/23 | 18:30 | Chelsea FC vs Liverpool FC | 2.70 | 3.50 | 2.35 |
| 15. 13/08/23 | 19:15 | Erzurumspor FK vs Bandirmaspor | 2.45 | 3.30 | 2.43 |
| 16. 13/08/23 | 20:00 | Estrela Amadora vs Vitoria SC Guimaraes | 2.65 | 3.10 | 2.60 |
| 17. 13/08/23 | 20:30 | Albacete Balompie vs Espanyol Barcelona | 2.95 | 3.15 | 2.35 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 11/08/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 18:00 | 1173 | Ural Yekaterinburg vs Spartak Moscow | 3.19 | 3.34 | 2.10 |
| 18:45 | 1318 | Frosinone vs Pisa | 1.73 | 3.71 | 4.38 |
| 19:00 | 2476 | Udinese vs Catanzaro | 1.41 | 4.50 | 6.91 |
| 19:00 | 2480 | TUS Bersenbruck vs Monchengladbach | 22.16 | 13.72 | 1.06 |
| 19:00 | 3407 | AL Salt vs Hussein Irbid | 5.40 | 3.60 | 1.53 |
| 19:00 | 3784 | Sandhausen vs Hannover | 3.17 | 3.49 | 2.19 |
| 19:00 | 4406 | Gornik Leczna vs Chrobry Glogow | 1.87 | 3.42 | 3.52 |
| 19:00 | 5160 | Saarbrucken vs Karlsruher SC | 3.50 | 3.66 | 1.99 |
| 19:30 | 3355 | FC Fredericia vs Hillerod | 1.72 | 3.63 | 3.93 |
| 19:55 | 3213 | Mladost Lucani vs Red Star Belgrade | 13.09 | 6.45 | 1.14 |
| 20:00 | 2375 | Copenhagen vs Odense | 1.46 | 4.65 | 5.66 |
| 20:00 | 3843 | FC Helsingor vs Aalborg | 4.63 | 3.83 | 1.58 |
| 20:00 | 4466 | HB Koge vs B 93 Copenhagen | 1.35 | 4.54 | 6.66 |
| 20:00 | 4685 | Amorebieta vs Levante | 3.27 | 3.12 | 2.16 |
| 20:30 | 1866 | Neuchatel Xamax vs FC Thun | 2.63 | 3.28 | 2.35 |
| 20:30 | 1896 | US Marignane vs Le Mans | 2.19 | 3.40 | 2.99 |
| 20:30 | 2640 | Stade Nyonnais vs FC Schaffhausen | 1.96 | 3.28 | 3.39 |
| 20:30 | 2861 | Almeria vs Rayo Vallecano | 2.46 | 3.38 | 2.87 |
| 20:30 | 4203 | Epinal vs Red Star | 2.89 | 3.25 | 2.31 |
| 20:30 | 4654 | Niort vs Avranches | 2.25 | 3.26 | 3.00 |
| 20:30 | 5122 | U Craiova SA vs Voluntari | 2.37 | 3.24 | 2.78 |
| 20:30 | 5280 | Dijon vs FC Rouen | 1.92 | 3.55 | 3.55 |
| 20:30 | 5317 | Cholet vs Chateauroux | 1.94 | 3.46 | 3.56 |
| 21:00 | 1141 | Al Ahli Jeddah vs AL Hazm | 1.36 | 4.82 | 7.76 |
| 21:00 | 1830 | Den Bosch vs FC Oss | 2.01 | 3.48 | 3.22 |
| 21:00 | 2043 | Groningen vs Jong Ajax | 1.70 | 3.72 | 4.18 |
| 21:00 | 3538 | Dordrecht vs NAC Breda | 3.22 | 3.48 | 2.01 |
| 21:00 | 4284 | Boluspor vs Adanaspor | 2.02 | 3.33 | 3.18 |
| 21:00 | 4888 | Trabzonspor vs Antalyaspor | 1.69 | 3.81 | 4.33 |
| 21:00 | 5113 | Cambuur vs Emmen | 2.62 | 3.24 | 2.48 |
| 21:00 | 5585 | De Graafschap vs ADO Den Haag | 1.96 | 3.47 | 3.37 |
| 21:00 | 5845 | FC Volendam vs Vitesse Arnhem | 3.17 | 3.56 | 2.03 |
| 21:15 | 3752 | FC Wil vs FC Sion | 2.98 | 3.33 | 2.11 |
| 21:30 | 1378 | Ramtha Club vs Faisaly Amman | 3.06 | 3.01 | 2.27 |
| 21:45 | 1386 | Shelbourne vs Shamrock Rovers | 4.35 | 3.39 | 1.71 |
| 21:45 | 2135 | The New Saints vs Gap Connahs Quay | 1.29 | 4.64 | 8.28 |
| 21:45 | 3522 | St Patricks vs Bohemians FC | 2.07 | 3.38 | 3.03 |
| 21:45 | 3736 | Eintracht Braunschweig vs Schalke 04 | 3.81 | 3.81 | 1.87 |
| 21:45 | 3844 | Cork City vs UCD Dublin | 1.35 | 4.44 | 6.86 |
| 21:45 | 4597 | Ballymena Utd vs Crusaders Belfast | 5.25 | 3.93 | 1.50 |
| 21:45 | 4664 | Dundalk FC vs Sligo Rovers | 2.05 | 3.29 | 3.14 |
| 21:45 | 4694 | Royal Antwerp vs Kortrijk | 1.30 | 5.16 | 8.14 |
| 22:00 | 2778 | Burnley vs Manchester City | 8.16 | 4.93 | 1.38 |
| 22:00 | 3254 | Nice vs Lille | 2.92 | 3.44 | 2.40 |
| 22:00 | 5458 | Genoa vs Modena | 1.50 | 4.05 | 6.24 |
| 22:15 | 2788 | Sporting Braga vs Famalicao | 1.44 | 4.22 | 6.56 |
| 22:15 | 4852 | Bologna vs Cesena | 1.33 | 4.89 | 8.33 |
| 22:30 | 4480 | Valladolid vs Sporting Gijon | 1.80 | 3.32 | 4.26 |
| 23:00 | 1244 | Sevilla FC vs Valencia | 1.98 | 3.45 | 3.91 |
| 23:15 | 5408 | UTC Cajamarca vs Carlos Mannucci | 1.75 | 3.43 | 4.03 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Ijumaa Agosti 11, 2023

Nipashe




Maguire mali ya West Ham UKURASA 22




Mshambuliaji wa Simba, Moses Phiri (juu kulia), akiwania mpira dhidi ya kiungo wa Singida Fountain Gate FC, Yusuph Kagoma, katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya pili ya michuano ya Ngao ya Jamii iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga jana. Simba ilishinda kwa penalti 4-2. **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**

# Simba, Yanga rasmi kukutana Jumapili

**Na Faustine Feliciane,** TANGA

## ●●● Ni katika fainali ya Ngao ya Jamii baada ya Mnyama...

YAMETIMIA, Simba itakutana na Yanga katika mechi ya fainali ya michuano ya Ngao ya Jamii itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini hapa baada ya jana kupata ushindi wa penalti 4-2 ilipokutana na Walima Alizeti, Singida Fountain Gate FC kutoka mkoani Singida.

**Yanga ambao ndio mabingwa watetezi wa taji hilo walitinga hatua hiyo juzi baada ya kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Azam FC.**

Timu hizo zililazimika kufika hatua ya matuta baada ya kutoka sare ya bila kufungana katika dakika 90 za kawaida na hivyo kuingia hatua hiyo ya kusaka mshindi.

Katika dakika 90 za kawaida, timu zote mbili zilishambuliana kwa zamu lakini hakuna aliyefanikiwa kutikisa nyavu za mpinzani wake huku Singida Fountain Gate wakionekana kucheza kwa nidhamu kubwa kwenye eneo lao la ulinzi.

Simba wanapaswa kujilaumu wenyewe baada ya kupoteza nafasi nzuri ya kufunga ndani ya dakika nne ya nyongeza baada ya kiungo wake, Saido Ntibanzokiza kupiga shuti hafifu la juu ambalo lilimlenga golikipa wa Singida FG, Beno Kakolanya.

Simba ikianza na mshambuliaji wake Mkongomani, Jean Baleke, ilishindwa kabisa kutumia nafasi walizozitengeneza kipindi cha kwanza katika dakika za nane kupitia kwa Willy Onana, dakika ya 33 Denis Kibu ambaye alikosa goli na dakika ya 39 Onana alikosa tena bao.

Hata hivyo hadi mwamuzi, Amina Kiando, kutoka Morogoro anapuliza kipenga cha kumaliza dakika 45 za kipindi cha kwanza, Singida FG ilionekana kufanya faulo nyingi ikilinganisha na Simba.

Licha ya kila timu kufanya mabadiliko katika kipindi cha pili, bado hayakusaidia kupata bao, Simba ikiwatoa Saido Kanoute na Baleke na nafasi zao kuchukuliwa na John Bocco na Fabrice Ngoma huku Singida FG wakimtoa France Kazadyi na nafasi yake kuchukuliwa Meddy Kagere.

Zikiwa zimesalia dakika nne mpira kumalizika Simba ilipata pigo baada ya beki wake, Henock Inonga, kuumia na hivyo Kenedy Juma aliingia kuchukua nafasi hiyo.

Golikipa wa Simba, Ally Salim, aliibuka shujaa baada ya kupangua penalti ya kwanza ya Singida FG iliyopigwa na Aziz Andambwile huku Kagoma akipaisha.

Kwa upande wa Simba waliofunga penalti ni Ntibazonkiza, Luis Miquissone, Mzamiru Yassin na Patrick Phiri.

Yanga inatetea taji hiyo baada ya mwaka jana kuwafunga watani zao Simba mabao 2-0 katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

# Gamondi: Mechi haikuwa nyepesi

**Na Faustine Feliciane,** TANGA

LICHA ya kupata ushindi wa mabao 2-0 katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya kwanza kuwania Ngao ya Jamii dhidi ya Azam FC, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema mchezo huo haukuwa mwepesi kutokana na wapinzani wao kuonyesha ushindani.

Mabao mawili ya dakika za jioni kutoka kwa Stephano Aziz Ki na Clement Mzize yaliipa Yanga ushindi na kutangulia hatua ya fainali.

Gamondi alisema ushindani walioupata umemsaidia kubaini 'kitu' ambacho atakwenda kukifanyia marekebisho watakaporejea kambini.

Kocha huyo alisema ililazimu kubadilisha mbinu zake mara kwa mara katika mchezo huo uliokuwa na ugumu uliotokana na ubora wa kikosi cha Azam.



"Haukuwa mchezo mwepesi hata kidogo, Azam walikuwa vizuri na walitupa changamoto kubwa, lakini nashukuru kwa ushindi huu ambao utatufanya tucheze fainali," alisema Gamondi.

Aliongeza anakwenda kufanyia kazi mapungufu katika mazoezi yatakayofanyika leo na kesho ili warejee wakiwa bora kwenye mechi ya fainali.

"Tulitengeneza nafasi nyingi sana za kufunga lakini hatukuzitumia ipasavyo, hili ni tatizo, lazima tuwe makini na nafasi tunazozipata, nimeliona hili na naenda kulifanyia kazi," alisema Gamondi.

Naye nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, alisema mechi hiyo ilikuwa ngumu kwa pande zote mbili.

Mwamnyeto alisema mabadiliko yaliyofanywa na kocha wao, yalisaidia kwa kiasi kikubwa kupata ushindi baada ya kumaliza kipindi cha kwanza bila ya kufunga bao.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >